




**Watanzania** Ukraine waanza kurejea nchini

UKURASA 3




**GUARDIOLA: SINA SHIDA GREALISH KUTOFUNGA**

UKURASA 22


# Nipashe

Alhamisi Machi 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580873

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

igital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




# Makamu wa Rais adai Katiba Mpya

UKURASA 2

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**EATV YAWATAMBUA WANAWAKE VINARA**

VITUO vya East Africa Radio na EATV, vimezindua mpango maalum wa...

UKURASA WA 4

**WADAIWA KUACHA MASOMO KWENDA KENYA KUCHUNGA**

BAADHI ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya...

UKURASA WA 5

**VIKAO 8 VYAMALIZA KERO 11 MUUNGANO**

VIKAO nane vimefanyika kwenye ngazi mbalimbali ili kuzitafutia ufumbuzi kero...




Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na baadhi ya viongozi mbalimbali wa dini baada ya kikao chao, Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## Diwani atajwa kesi ya mauaji dada wa bilionea Msuya

UKURASA 3



## Makonda aiomba mahakama siku 21 kujibu hoja kesi yake

UKURASA 2

**MICHEZO** **PABLO ATANGAZA VITA MPYA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# HABARI KITAIFA




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akifungua mkutano wa nne wa mwaka wa uongozi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) na mahafali ya awamu ya 7 ya mafunzo ya mwanamke kiongozi, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako na Mkurugenzi Mtendaji wa ATE, Suzanne Ndoba. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Makamu wa Rais adai Katiba Mpya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ameandaa waraka wa mapendekezo tisa kwa ajili ya kuimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa na kuyawasilisha kwa Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Vilevile, amesema kuna haja Tanzania kuwa na Katiba Mpya kwa kuwa katiba ya sasa ina upungufu ambao anaona kunahitajika kufanyiwa marekebisho.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kwenye Hoteli ya Golden Tulip mjini Zanzibar ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya mwaka mmoja wa uongozi wake tangu alipoteuliwa kushika wadhifa huo kufuatia kifo cha Maalim Seif Sharif Hamad.

Alisema Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni muhimu kwa kuwa ni matakwa ya wananchi na sio ya chama na kwamba katiba ya sasa ina upungufu, hivyo inahitajika kufanyiwa marekebisho.

"Maoni ya wananchi yalishakusanywa kupitia Tume ya Jaji (Joseph) Warioba, iliyopita nchi nzima kukusanya maoni ya Watanzania ya namna ya katiba wanayoitaka iwaongoze, lakini bahati mbaya mchakato ule uliharibika katikati kwa kubadilishwa na wanasiasa," alisema.

Kuhusu mapendekezo yake tisa, Makamu wa Rais alisema yakisikilizwa na kufanyiwa kazi, yataimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa ikiwamo kurejesha imani kwa wananchi na kuaminiana ambapo imani hiyo hivi sasa ipo zaidi kwa viongozi wa juu wa kitaifa pekee. Alisema lazima kuanzishwe tume ya kusimamia utekelezaji wa maridhiano, mapendekezo juu ya namna ya kuimarisha mfumo wa vyombo vya kutoa haki kama mahakama na mfumo wa sheria za kiutawala.

Mapendekezo mengine aliyoyaainisha katika waraka huo ni kujenga utengamano wa kijamii, kuleta utengamano wa kisiasa, uhuru na ustaarabu katika kuendesha siasa, kupitia na kujenga upya mfumo wa uchaguzi.

Alibainisha mambo mengine yaliyomo kwenye waraka huo ni uendeshaji wa serikali kuu, wakala na mashirika yake kwa kuzingatia gharama za uendeshaji wa serikali pamoja na ukubwa wake ili kukuza ufanisi na gharama bora ya rasilimali za umma. "Mengine ni mapendekezo juu ya mfumo wa kitaasisi wa kusimamia na kuendelea mfumo wa maridhiano ya kitaifa endelevu. Haya ni baadhi tu ya mambo ya msingi ambayo yamependekezwa katika waraka huo," alisema.

Alisema dosari zilizoko katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa inaonekana katika ngazi ya juu pekee kwa viongozi wa kitaifa na Baraza la Mawaziri, lakini bado maeneo mengine haijafanya kazi na kutolea mfano nafasi za udiwani wa viti maalumu pamoja na uenyeviti wa mabaraza ya miji na halmashauri.

"Kuna nafasi ya uteuzi wa viti maalumu vya udiwani lakini tulitegemea nafasi hizo zitashirikisha vyama viwili vinavyounda serikali lakini halikufanyika hilo. Hii haijengi, inabomoa na inaturejesha nyuma," alisema Othman.

Othman ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, alisema malengo ya baadaye ya chama chake ni kuitazama Zanzibar kwa umuhimu wake, akisisitiza inastahiki kuwa mbali zaidi kuliko ilipo sasa.

"Sisi hatutazami uchaguzi wa mwaka 2025 kama tupo katika siasa za ligi (ushindani wa kisiasa), bali tunaitazama Zanzibar kwamba kuna fursa mbalimbali ambapo itachukua muda kuzitengeneza fursa hizo endapo zitapotea," alisema.

# 'TRA wekeni mazingira wezeshi ulipaji wa kodi'

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru, amewataka wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kuweka mazingira wezeshi kwa walipakodi ili kuongeza mapato ya serikali.

Mafuru alisema hayo kwenye hotuba yake alipomwakilisha Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamadi Hamadi Chande, kwenye uzinduzi wa Baraza Kuu la kwanza la Wafanyakazi wa TRA uliofanyika jana jijini hapa.

Aliwataka wafanyakazi wa TRA kuhakikisha wanaweka mazingira rafiki kwa walipakodi ili kuongeza mapato ya serikali.

"Ninapenda kuwakumbusha agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu kutekeleza majukumu yetu kwa weledi na uadilifu wa kiwango cha juu na pia kukutana na wafanyabiashara kwa lengo la kusikiliza na kutatua matatizo yao ili kuongeza mapato ya serikali," alisema.

Kamishna wa Mkuu wa (TRA) na Mwenyekiti wa Baraza hilo, Alphayo Kidata, alisema baraza hilo ni la kwanza tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 1996.

Kidata alisema uhusiano mzuri walionayo watumishi wa TRA ni sababu ya kuendelea kuwapo na kuimarika kwa mamlaka hiyo na kuongezeka kwa makusanyo mwaka hadi mwaka.

Alisema wastani wa makusanyo kwa mwezi katika mwaka wa kwanza wa shughuli za mamlaka hiyo mwaka 1996/97 yalikuwa Sh. bilioni 42 na kwa sasa wastani wa makusanyo kwa mwezi ni Sh. trilioni 1.85.

Alikumbusha kuwa Desemba 2021, TRA ilifanikiwa kukusanya Sh. trilioni 2.5 ikiwa ni kiwango cha juu zaidi ya makusanyo yote ya mwezi tangu uhuru wa nchi.

# Paul Makonda aiomba mahakama siku 21

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, ameiomba Mahakama ya Hakimu Mkazi Kinondoni jijini Dar es Salaam impe muda wa kujibu maombi yaliyofunguliwa na mwanahabari, Saed Kubenea, ya kutaka kumfungulia kesi ya jinai.

Maombi hayo yaliwasilishwa jana mbele ya Hakimu Aron Lyamuya na Wakili wa Makonda, Goodchance Reginald, aliyedai amechelewa kupata wito huo kwa kuwa ameupata kupitia vyombo vya habari.

"Mteja wangu ameni-engage hivi karibuni kwamba hakupata taarifa yoyote ya summons (wito), ingependeza tungepata summons na muda wa kujibu," alidai Wakili Reginald.

Ombi hilo lilipingwa na Hekima Mwasipu, Wakili wa Kubenea aliyedai hajaiambia mahakama Makonda alipataje taarifa hadi amemtuma afike kumwakilisha mahakamani huko.

Wakili Reginald alijibu pingamizi hilo akidai "mteja wangu alipata hizi habari kupitia vyombo vya habari, akaona si vyema yeye alikuwa kiongozi wa serikali, akaona ni vyema alete wakili lakini summons hajapewa."

Kutokana na maombi hayo, Hakimu Lyamuya alimpa siku 21 Makonda ili kuwasilisha hati kinzani dhidi ya maombi hayo yaliyofunguliwa na Kubenea.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Subira Mwalumuli, alidai mahakamani huko kuwa wajibu maombi namba moja na mbili, ambao ni Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), wanatarajia kuleta mapingamizi ya awali dhidi ya maombi hayo.

"Shauri liko kwa ajili ya kutajwa lakini pia tarehe hii ilipangwa kuletwa hati kinzani kwa wajibu maombi wa kwanza na wa pili wameleta taarifa ya kutoa pingamizi la awali na pingamizi hili la awali ni juu ya shauri lililo mbele ya mahakama yako. Kwa hivyo, tunaomba kutoa hiyo taarifa mbele ya mahakama yako," alidai Wakili Mwalumuli.

Hakimu Lyamuya aliahirisha kesi hiyo hadi Machi 25, mwaka huu, huku upande wa wajibu maombi namba moja na mbili, yaani DPP na Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) wakidai wanakusudia kuleta pingamizi la awali juu ya maombi hayo.

Katika kesi hiyo, Kubenea anawakilishwa na jopo la mawakili wakiongozwa na Nyaronyo Kicheere na Hekima Mwasipu.

Kwa mujibu wa hati ya mashtaka, Makonda anadaiwa kuwa siku ya tarehe 17, Machi 2017, akiwa na watu waliobeba silaha za moto, alivamia kituo cha Clouds TV na kumwagiza mtangazaji wa kipindi cha Shilawadu kurusha video inayomwonyesha mwanamke (jina tunalihifadhi) aliyedaiwa kuonekana akifanya tendo la ndoa na mmoja wa viongozi wa dini nchini (jina tunalihifadhi).

Kwa mujibu wa hati ya kiapo ya Kubenea, anadai kitendo cha Makonda kuvamia kituo cha televisheni, tena akiwa ameongozana na askari waliobeba silaha za moto, ni kinyume cha Sheria ya Kielektroniki na Posta ya Mwaka 2010.

Maombi ya kutaka kumshtaki Makonda yaliwasilishwa mahakamani chini ya kifungu cha 99 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai, Sura ya 20.

Mbali na Makonda, wengine waliotwa mahakamani ni DCI na DPP wanaotuhumiwa wameshindwa kuchukua hatua za kumfungulia mashtaka ya jinai mtuhumiwa huyo.

# Watanzania Ukraine waanza kurejea nchini

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imetuma maofisa wake walioko katika balozi za Sweden na Ujerumani kwenda katika nchi za Poland na Hungary kusimamia taratibu za kuwawezesha wanafunzi wa Kitanzania walioko Ukraine kuvuka mpaka na kuingia katika nchi hizo kiurahisi.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alitangaza hatua hiyo jana jijini Dar es Salaam alipokutana kwa mazungumzo na Kamati ya Wazazi wa Wanafunzi Wanaosoma Ukraine kuwatia moyo na kueleza hatua zinazoendelea kuchukuliwa za kuwawezesha kurejea nchini salama.

Taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari na Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano ya Serikalini katika wizara hiyo, Emmanuel Buhohela, ilibainisha kuwa Balozi Mulamula aliiambia kamati hiyo kuwa serikali inafanya mazungumzo na Ubalozi wa Russia nchini ili kuweka mazingira salama ya kwa wanafunzi wa Kitanzania waliokwama Ukraine ili waondoke kwa kutumia mpaka wa Russia.

Alisema hiyo ni kutokana na kutokuwa na njia mbadala na kuwataka wazazi kuwatuliza watoto wao wanapopata fursa ya kuzungumza nao ili kuwaepusha na taharuki.

Balozi Mulamula pia alitumia fursa hiyo kuwaondoa hofu wazazi wa wanafunzi takribani 160 wanaosoma katika Mji wa Sumy ambao uko mpakani mwa Ukraine na Russia kwa kuwaeleza kwamba wameshauriwa kubaki katika vyuo vyao kwa sababu za kiusalama.

Alisema uongozi wa chuo chao umeahidi kuwapatia mahitaji na huduma muhimu za kibinadamu ikiwa ni pamoja na chakula, malazi na matibabu. "Kwa sasa wanafunzi wengi wameondoka Ukraine kuelekea nchi za Poland, Romania na Hungary ambapo hadi Machi Mosi, 2022, wanafunzi 38 walifanikiwa kuingia Poland na kupatiwa visa ya siku 55 inayowaruhusu kuwapo Poland kwa siku hizo wakati wakijiandaa kurejea nchini au kwingineko," alibainisha.

Pia alisema wanafunzi 71 wamefanikiwa kuingia Hungary na kati yao, 11 wameondoka kurejea Tanzania huku mmoja akibaki Hungary baada ya kukutwa na maambukizi ya UVIKO-19 na wengine wameelekea kwenye mataifa mengine kwa ndugu na jamaa zao. "Wanafunzi wawili wamefanikiwa kuingia Romania ambapo mmoja kati yao ameondoka kurejea Tanzania, mmoja ameingia Slovakia na mwingine Denmark," alisema.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolph Mkenda, aliiambia kamati hiyo kuwa serikali itaangalia namna ya kuandaa utaratibu maalumu wa kuwawezesha wanafunzi hao kuendelea na masomo wawapo nchini kwa kuwa ni azma yake kuwapeleka wengi nje ya nchi kusoma.

Mwenyekiti wa kamati hiyo ya wazazi wanaosoma Ukraine, Wakili John Choma, akizungumza kwa niaba ya wazazi, alishukuru serikali kwa namna anavyolishughulikia suala hilo na kuwataka wazazi na Watanzania kwa ujumla kuwa watulivu wakati suala hilo likifanyiwa kazi.



Mkuu wa Wilaya ya Biharamulo mkoani Kagera, Kemilembe Lwota (wapili kulia), akigawa miche ya kahawa ya robusta kwa wakulima wa wilaya hiyo jana, iliyozalishwa na Kampuni ya JJAD Kagera Farmers (T), kwa ufadhili wa Bodi ya Kahawa nchini (TCB). Habari Uk. 08. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Diwani Athumani atajwa kesi mauaji dada wa Bilionea Msuya

**Na Kulwa Mzee**

OFISA wa Polisi, Mrakibu (SP) Latifa Mohammed, amedai hafahamu kama aliyekuwa Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI), Kamishna Diwani Athumani, ndiye alitoa maelekezo mke wa marehemu Bilionea Msuya, Miriam Mrita, arekodiwe video.

Pia amedai kuwa hafahamu kama CP Diwani ni kaka wa marehemu Aneth Msuya na hafahamu kama alikuwa akiongoza migogoro ya ndugu.

SP Latifa alidai hayo jana Mahakama Kuu mbele ya Jaji Edwin Kakolaki wakati akitoa ushahidi kwenye kesi ya mauaji inayomkabili Miriam na mwenzake ambao wanadaiwa kumuua dada wa Bilionea Msuya, Aneth Msuya.

Akiongozwa na Wakili wa Utetezi, Peter Kibatala, alidai alikwenda Arusha Agosti 4, 2016 kwa ajili ya kumkamata Miriam kwa tuhuma za mauaji yaliyotokea maeneo ya Kibada, Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Alidai kuwa katika safari yake aliongozana na SP Jumanne Malangahe na Mrakibu Msaidizi (ASP) David Mhanaya lakini hafahamu kama Jumanne anajulikana nchi nzima kwa kutesa watuhumiwa.

Shahidi alidai kuwa alikuwa anafahamu jina la aliyekuwa anakwenda kumkamata na tuhuma za mauaji zinazomkabili. Pia alidai alimkamata maeneo ya Tembo Club lakini hakuwa na hati ya kumkamata, akidai kifungo namba 14 cha Sheria ya Makosa ya Jinai (CPA) kilimruhusu.

Wakili Kibatala alimpa sheria hiyo asome kifungu kilichomruhusu lakini shahidi alikaa kimya kwa dakika kadhaa bila majibu.

Kibala alisoma kifungu kimoja baada ya kingine lakini hakukuwa na kifungu wala mazingira yaliyoruhusu SP Latifa kumkamata mtuhumiwa bila hati ya ukamataji.

Shahidi alidai walikuwa na hati ya upekuzi, baada ya kumkamata walikwenda kufanya upekuzi nyumbani kwake maeneo ya Sakina, Arusha.

Pia alidai kuwa katika upekuzi walichukua nguo aina ya suti jozi mbili, viatu jozi mbili na kadi za magari lakini hajui magari hayo yalihusikaje katika tukio la mauaji.

Shahidi alidai kuwa alimhoji mshtakiwa kwa mdomo huku ASP David akichukua video wakati wa mahojiano hayo lakini akadai kuwa katika kifungu namba 57 cha CPA, hakuna mahali palipoandikwa mahojiano yachukuliwe kwa kurekodi video isipokuwa kuna palipoandikwa mahojiano kwa njia ya mdomo.

Wakili Kibatala alihoji kama shahidi anafahamu kuwa maelekezo ya kumrekodi video mshtakiwa Miriam yalitoka kwa aliyekuwa DCI wakati huo, Kamishna Athumani.

Kibatala alihoji kama anafahamu kuwa Diwani ni kaka wa marehemu Aneth Msuya na akahoji kama anafahamu kuwa migogoro ya ndugu ilikuwa ikiongozwa na Athumani.

Shahidi alidai hafahamu kama David alipewa maelekezo na Kamishna Diwani Athumani kurekodi video na hafahamu kama ni kaka wa marehemu Aneth Msuya na hafahamu kama alikuwa akiongoza migogoro ya ndugu.

SP Latifa alidai walikamata gari aina ya Suzuki Vitara lenye namba za usajili T620 CBB, gari T677 BNM Toyota Landcruiser na T800 CKF Range Rover lakini hajui yalihusikaje katika tukio la mauaji.

Wakati akihojiwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Geses Tesha, shahidi alidai walikwenda kumkamata mtuhumiwa Agosti 4, 2016 Arusha na Agosti 5 walimkamata Tembo Club.

Alidai baada ya kumkamata walikwenda kufanya upekuzi nyumbani kwake, walichukua nguo na viatu na baada ya kukamilisha upekuzi walirejea Dar es Salaam .

Latifa alidai walimfikishia Kituo cha Polisi Chang'ombe na Agosti 8, 2016 walifanya mahojiano naye kwa mdomo na kwa kumrekodi video. Alidai kuwa Afande David alikuwa akirekodi video, mtuhumiwa alieleza mpango mzima wa mauaji, alionyesha maeneo waliyokuwa wanakutana kabla ya tukio na baada ya tukio la mauaji maeneo ya Kibada.

Katika kesi hiyo ya mauaji washtakiwa ni mke wa marehemu bilionea Erasto Msuya, Miriam Mrita na mfanyabiashara, Revocatus Muyella.

Katika kesi ya msingi namba 103/2018, washtakiwa hao wanadaiwa kumuuwa kwa kukusudia Aneth Msuya, dada wa marehemu bilionea Msuya Mei 25, 2016 maeneo ya Kibada, Kigamboni, Dar es Salaam.


## TANGAZO TANGAZO TANGAZO

PAMOJA AUCTION MART AND COMPANY LTD NA TRUST RECOVERIES LTD WATAENDESHA MINADA YA HADHARA YA KUUZA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU WA **LETSHEGO BANK TANZANIA LIMITED** KUANZIA 16/03/2022 HADI 14/05/2022 MUDA NI KUANZIA SAANNE ASUBUHI NA KUENDELEA

| NA | JINA LA MDAIWA/MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | JINA LA DALALI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | AGUSTINO GERVAS KOMBA | NYUMBA PLOT NO.844 BLOCK HH ISYESYE MBEYA | ISYESYE MBEYA | 16/03/2022 | PAMOJA AUCTION MART AND COMPANY LTD |
| 2. | AGUSTINO GERVAS KOMBA | GARI NO T.380 BRN LAND CRUISER PRADO | ISYESYE MBEYA | 16/03/2022 | PAMOJA AUCTION MART AND COMPANY LTD |
| 3. | MUSSA DAUDI MWASHEMELE | NYUMBA PLOT NO.38 NA 40 BLOCK G MPEMBA TUNDUMA | MPEMBA TUNDUMA | 18/03/2022 | PAMOJA AUCTION MART AND COMPANY LTD |
| 4. | ALBERT NYALUKA | NYUMBA PLOT NO.34268 MBYLR | MAJENGO TUNDUMA | 19/03/2022 | TRUST RECOVERIES LTD |
| 5 | LILIAN J NILSEN | NYUMBA PLOT NO.24274 MBYLR | TUNDUMA | 2/04/2022 | TRUST RECOVERIES LTD |
| 6. | ABU MWASHIMBU | NYUMBA PLOT NO.41852 MBYLR | KABWE MBEYA MJINI | 16/04/2022 | TRUST RECOVERIES LTD |
| 7. | FERDINAND KIKOTI | NYUMBA PLOT NO.36080 MBYLR | IRINGA MJINI | 30/04/2022 | TRUST RECOVERIES LTD |
| 8. | DIONIS MGAYA | NYUMBA PLOT NO.2521 MBYLR | MWAKIBETE-MBEYA -MJINI | 14/05/2022 | TRUST RECOVERIES LTD |

**MASHARTI YA MNADA;**

1. DHAMANA ZITAUZWA KAMA ZILIVYO, MNUNUZI ATALIPIA 25% YA BEI YA MNADA. 75% ITALIPWA NDANI YA SIKU 14 KUTOKA SIKU YA MNADA. AKISHINDWA KULIPA, MALIPO YA AWALI HAYATARUDISHWA.
2. GHARAMA ZA KUBADILISHA HATI ZA UMILIKI ZITAKUWA JUU YA MNUNUZI.
3. UKAGUZI WA DHAMANA ZINAZOUZWA UTAANZA SIKU MOJA KABLA YA MNADA NA GHARAMA ZA KUMPELEKA MTEJA KWENYE DHAMAN ZITAKUWA JUU YA MTEJA.

*KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NA:-*

**TRUST RECOVERIES LIMITED: 0742674672 OR 0678799566**
**PAMOJA AUCTION MART AND COMPANY LTD: 0755366977 OR 0715604560**

216729201

# EATV yawatambua kwa tuzo wanawake vinara mwaka 2022

Na Christina Mwakangale

VITUO vya East Africa Radio na EATV, vimezindua mpango maalum wa kuwatambua wanawake ambao hawajatambulika licha ya kuwa na mchango mkubwa kwenye jamii, kwa kuwapatia vyeti kupitia kampeni ya Mwanamke Kinara 2022.

Kampeni hiyo ambayo itafanyika mwezi huu ni maalumu kwa ajili ya kusherehekea mwezi ulioteuliwa kwa ajili ya Siku ya Mwanamke Duniani, inayoadhimishwa kila mwaka.

Akizungumza kwenye uzinduzi huo ulioshirikisha wanawake tofauti wakiwamo wabunge, madiwani na wakuu wa vitengo kwenye taasisi binafsi na umma, Ofisa Mkuu wa Masoko wa EATV, Evelyne Ngalo, alisema lengo la kampeni ni kutambua kinachofanywa na wanawake hao.

Alisema kwenye jamii kuna wanawake ambao tayari wanatambulika na kupata umaarufu katika nyanja tofauti, na kwamba ambao hawajatambulika ni fursa yao kupitia kampeni hiyo ambayo kilele chake ni Machi 19, mwaka huu.

"Kwenye jamii kila mwanamke ana mchango wake katika ujenzi wa familia kiuchumi na jamii haijawatambua, wapo pia ambao tunawatambua. Kampeni hii tutajikita kumwinua mwanamke huyu ambaye hajatambulika awe mjasiriamali au shughuli yoyote.

"Tutatoa vyeti kwa wanawake hawa na pia kutakuwa na maonyesho ya bidhaa mbalimbali za kazi za wanawake watakaoshiriki siku ya kufunga kampeni Machi 19, mwaka huu. Mwanamke ni nguvu kubwa hata hapa EATV, kwenye nafasi za uongozi ni 50/50," alisema Ngalo.

Janeth Mahawanga, Mbunge Viti Maalum, alisema wanawake wanaendelea kupata fursa kutokana na kutambuliwa mchango wao, na kwamba Sh. bilioni 3.9 zimetengwa kwa Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mkurugenzi wa Masoko wa TBL Plc, Doreen Tumurebire, alisema kampuni hiyo inatoa kipaumbele kwa wanawake, na kwamba sehemu kubwa bidhaa wanazonunua ni kutoka kwenye mashamba ya wanawake.

"Tunahitaji jumuiya ambayo ina uongozi shirikishi na usawa ili kuendelea, hata kiongozi wetu ni mwanamke, wakurugenzi wetu pia wanawake," alisema Doreen.

Mkuu Mawasiliano na Masoko Benki ya UBA, Blendansia Kileo, alisema asilimia 40 ya wanawake kwenye taasisi hiyo ni viongozi, huku akisisitiza kwamba pia wanaume ambao wanawasaidia wanawake kufanikiwa maradufu wana sababu ya kupongezwa.




Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Dar es Salaam, Janeth Mahawanga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni ya mwanamke kinara inayoendeshwa na Kituo cha Televisheni cha East Africa (EATV) na Radio, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam juzi jioni, yenye lengo la kuwaibua wanawake wajasiriamali wanaofanya vizuri lakini hawatambuliki. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wadaiwa kuacha masomo kisha kwenda Kenya kuchunga mifugo

Na Zanura Mollel, LONGIDO

BAADHI ya wanafunzi wa shule za msingi na sekondari katika Wilaya ya Longido mkoani Arusha, hasa wanaotoka jamii ya kifugaji ya Kimasai, wanadaiwa kuacha masomo na kutimkia nchi jirani ya Kenya, kutafuta ajira za kuchunga mifugo na kazi za ulinzi.

Mkuu wa Wilaya ya Longido, Nurdin Babu, amethibitisha kuwa tayari ameshapokea taarifa juu ya jambo hilo, akiahidi kuzifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili kudhibiti wimbi hilo.

Habari kuhusu wanafunzi hao kuingia katika ajira za watoto, zilifichuliwa jana na mwanaharakati wa haki za binadamu ambaye ni Mkazi wa Longido, Sambeke Saning'o.

Saning'o alisema hivi sasa kuna kundi kubwa la watoto, hasa wanafunzi wilayani humo wanaotoroka nyumbani na kwenda nchini Kenya, kufanya kazi ya kuchunga mifugo pamoja na kazi za ulinzi.

"Hao watoto wanaoacha masomo yao wanakimbilia nchi jirani ya Kenya, maeneo ya Loita na Kajiado kwa ajili ya kutumikishwa kikazi. Kama wanaharakati, hatukubaliani na uamuzi wa baadhi ya wazazi kushindwa kuwalinda watoto wao au kuruhusu watoto kwenda kutafuta kazi, huku wakiacha masomo yao, tena wakiwa wana umri mdogo.

"Watoto hao wanapofika nchi ya Kenya, hudanganya majina yao na maeneo waliyotokea, hususani upande wa Tanzania, lakini wanaenda mbali zaidi kwa kudanganya koo zao na hata majina ya wazazi wao.

"Tunapotambua mtoto ametoroka, tunafanya utaratibu wakuwatafuta kwa kutembea na picha maeneo ya mpakani, lakini hatufanikiwi kuwapata kutokana na majina yao tunayoyafahamu.

"Mimi mwenyewe ni shahidi mzuri wa hili linaloendelea la watoto kutafuta ajira za kuchunga mifugo na kazi za ulinzi, kwa maana nimeenda kumfuatilia mtoto wangu aliyekuwa ametoroka kwenda Kenya, alikuwa ni mwanafunzi wa darasa la sita wa Shule ya Msingi Longido (12)," alisema. "Kuna sehemu nimekuta watoto si chini ya 100 wa kitanzania, wenye umri wa kwenda shule, nimewakuta huko Kenya wanafanya kazi. Nashauri tufanye sensa kubaini watoto waliotoroka ni wangapi hapa wilayani na tutawapataje," aliongeza.

Naye Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Longido, Atunagile Chisunga, alipoulizwa sheria inasemaje kuhusu ajira za watoto alisema: "Sheria haijatoa kibali cha watoto kuajiriwa. Mtoto ni kuanzia umri wa miaka 18 kushuka chini, kumpa kazi mtoto chini ya miaka hiyo, tunatafsiri kama utumikishwaji kikazi.

"Kama halmashauri, bado hatujaanza kushughulikia, kwa sababu tunasikia tu mzazi akisema mtoto katoroka kaenda Kenya, lakini hawaleti taarifa rasmi ofisini.

"Lakini walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari, hawajatupa taarifa za watoto walioacha shule, nitawaandikia barua ili nipate taarifa za watoto ambao hawapo shule na hawajulikani walipo."

Mbunge mstaafu wa Longido, Lekule Laizer akizungumzia tatizo hilo, alisema kwa sasa hali ni tete, ndani ya jamii ya kifugaji ya Kimaasai, kwa kuwa watoto wamekuwa kama machokora na kwamba kuna umuhimu wa kutafuta njia sahihi ya kukabiliana na hali hiyo.

Mwaka jana, wakati Mrakibu wa Jeshi la Uhamiaji nchini, Azizi Kirondomali, akitoa mafunzo kwa viongozi mbalimbali wa mpaka wa Namanga unaozitenganisha nchi za Tanzania na Kenya, alisema vitendo hivyo ni sawa na biashara haramu ya binadamu au usafirishaji haramu wa binadamu.

## Serikali yataka nafasi zaidi kwa wanawake

Na Romana Mallya

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amezitaka kampuni kuongeza idadi ya wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi ili washiriki kutoa maoni na uamuzi kwa kuwa utafiti unaonyesha uwapo wao huongeza ufanisi na uzalishaji sehemu za kazi.

Hayo yamo katika hotuba yake iliyosomwa jana jijini Dar es Salaam na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, wakati wa mkutano mkuu wa nne wa uongozi wa Chama cha Waajiri Tanzania (ATE) uliofanyika sambamba na mahafali ya saba ya programu ya mwanamke kiongozi, wanawake 43 wakihitimu.

Mkutano huo ambao umeandaliwa na ATE kwa kushirikiana na Vyama vya Waajiri Norway (NHO), ulibebwa na ujumbe usemao "Usimamizi wa Mabadiliko ya Tabianchi; Usawa kwa Maendeleo ya Sasa na Baadaye".

Katika mkutano huo, pia kulikuwa na uzinduzi wa kanzidata ya wanawake ambao wamepitia programu hiyo ili kutoa fursa kwa serikali, taasisi na idara kuwatumia pindi watakapokuwa na uhitaji huo, ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya mwaka jana.

Dk. Mpango alisema ATE kwa kushirikiana na serikali wana nia thabiti kuhakikisha wanafikia usawa wa kijinsia katika nafasi za juu za uongozi wa kampuni na katika bodi mbalimbali.

"Nimeambiwa kuwa wanawake kadhaa waliohitimu programu hii tayari wamefanikiwa kupata nafasi za juu za uongozi na pia kuwa wawakilishi kwenye bodi mbalimbali huku mchango wao ukionekana dhahiri," alisifu.

Kiongozi huyo alisema licha ya wanawake kuwa mstari wa mbele katika kuyatunza mazingira, wao ndiyo waathirika wakubwa wa matokeo yake.

Alisema Rais Samia amekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha nchi haibaki nyuma katika kushiriki juhudi za kikanda na za kimataifa za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema mabadiliko ya sayansi na teknolojia, kuwapo kwa namna mpya za uharibifu na uchafuzi wa mazingira pamoja na mikataba mipya ya kikanda na kimataifa juu ya utunzaji wake, yamewalazimisha kukaa mezani kuandaa sera mpya iliyozinduliwa mwezi uliopita. "Taarifa Na. 3 ya mwezi Agosti 2019 juu ya Hali ya Mazingira ilionyesha uharibifu wa ardhi umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 1980 hadi asilimia 50 mwaka 2012 na asilimia 63 mwaka 2018, hali ambayo ni hatari kwa vizazi," alionya.

Dk. Mpango alisema Rais Samia alikuwa mmoja wa marais wa kwanza watatu waliotia saini 'Glasgow Women's Leadership Statement' ambayo inatoa wito kwa nchi kuunga mkono uongozi wa wanawake na mabinti katika masuala yote ya tabianchi katika ngazi zote za kisiasa na kijamii.

"Tunatambua bado ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi katika masuala haya sio wa kuridhisha. Hii inachagizwa na mambo mengi kama vile elimu na uelewa wa mambo haya," alisema.

Dk. Mpango alizihimiza kampuni kuendelea kuhakikisha wanaongeza idadi ya wanawake kwenye nafasi za juu za uongozi ili kuwapa nafasi ya kushiriki kutoa maoni na uamuzi kwa kuwa na mtazamo wao juu ya mazingira.

Alizitaka kampuni kushirikiana na serikali kufuata sheria zilizowekwa juu ya kuhifadhi na kutunza mazingira pamoja na kujitoa kitaalamu na kifedha katika kuunga mkono juhudi za kuyatunza.

## HABARI KITAIFA



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Lawrence Mafuru (kushoto), akikata utepe kuzindua rasmi Baraza Kuu la kwanza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo 1996, katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma jana. Kulia ni Kamishna Mkuu wa TRA na Mwenyekiti wa kwanza wa Baraza hilo, Alphayo Kidata. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

### MWAKA MMOJA SAMIA IKULU:

# Vikao nane vilivyomaliza kero 11 Muungano

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIKAO nane vimefanyika kwenye ngazi mbalimbali ili kuzitafutia ufumbuzi kero 11 kati ya 18 za Muungano ndani ya kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi hicho.

Aliweka wazi vikao hivyo ni cha Kamati ya pamoja ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Hafla ya kusaini Hati za Makubaliano ya kuondoa hoja zilizopatiwa ufumbuzi, Kikao cha Mawaziri wa JMT na SMZ.

Vingine ni cha Makatibu Wakuu wa JMT na SMZ, Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara ngazi ya Makatibu Wakuu, Kikao cha Kamati ya Fedha, Uchumi na Biashara, Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ na Kikao cha Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya JMT na SMZ.

Alisema katika kipindi hicho vimefanyika vikao hiyo ambavyo vilijadili kwa kina hoja hizo na kuzipatia ufumbuzi na kuondolewa kwenye orodha ya hoja.

Alitaja hoja hizo ni uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar, usimamizi wa ukokotoaji na ukusanyaji wa Kodi kwenye Huduma za Simu unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRB), mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Barabara ya Chake chake hadi Wete – Pemba, mkataba wa mkopo wa fedha za mradi wa ukarabati wa hospitali ya Mnazi Mmoja.

Nyingine ni Mkataba wa mkopo wa fedha za ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri, uvuvi kwenye Ukanda wa Uchumi wa Bahari Kuu, Ajira kwa Watumishi wa Zanzibar katika Taasisi za Muungano.

Pia alisema mgawanyo wa mapato yatokanayo na Misaada kutoka Nje ya Nchi, Mapato yanayokusanywa na Uhamiaji kwa upande wa Zanzibar, Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Tanzania Revenue Appeal Tribunal (TRAT) kutoka Zanzibar na uteuzi wa Mjumbe wa Bodi ya Bima ya Amana (DIB) kutoka Zanzibar.

Fedha za Uviko-19

Jafo alisema Zanzibar imepatiwa Sh. bilioni 230 kati ya Sh.Trilioni 1.3 zilizotokana na mkopo nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kukabiliana na athari za UVIKO-19.

Alisema fedha hizo zimeelekezwa kwenye huduma za kijamii zikiwamo afya, elimu, miundombinu na ujenzi wa masoko.

Pia alisema miradi na programu zingine ni Mpango wa kunusuru kaya Maskini Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili uliozinduliwa mwezi Februari, 2020 ambapo Sh. bilioni 112.9 zitatumika Zanzibar.

Waziri Jafo alisema kwa kipindi hicho Serikali imefanya vikao 21 vya kuimarisha ushirikiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar kwenye sekta za nishati, maji, madini, uchukuzi, utumishi na utawala bora, uratibu wa shughuli za Serikali, viwanda na biashara.

Nyingine ni maliasili na utalii, afya, kilimo, habari, utamaduni, sanaa na michezo, ardhi, fedha na mipango na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Alisema kwa kipindi hicho Ofisi hiyo imetunga na kuboresha Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo ikiwamo Sera ya Mazingira ya mwaka 2021, Kutunga Kanuni za Udhibiti wa Taka za Kieletroniki za mwaka 2021, Kuandaa Mkakati wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (2021-2026).

Kadhalika, alisema mikataba na itifaki mbalimbali zimeridhiwa ikiwamo mkataba wa Minamata kuhusu udhibiti wa zebaki.

Jafo alisema Ofisi hiyo imefanya tathmini ya awali ili kubaini uharibifu wa mazingira uliopo katika baadhi ya fukwe nchini.

# Polisi wamganda 'Mfalme' Zumaridi

**Na Richard Makore, MWANZA**

JESHI la Polisi mkoani Mwanza limeendelea kumshikilia Mchungaji Diana Bundala, maarufu Zumaridi, aliyekamatwa wiki iliyopita kwa tuhuma za kufanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramadhani Nganzi, alipotafutwa na Nipashe juzi kuzungumzia hatima ya mtuhumiwa huyo, alijibu kwa kifupi kwamba bado upelelezi unaendelea na utakapokamilika atapelekwa mahakamani.

Kwa mujibu wa Kamanda Ng'anzi, Mfalme Zumaridi alikamatwa nyumbani kwake akidaiwa kuwa na watu 149 waliokuwa wakiishi kwake.

Mchungaji huyo mwenye umri wa miaka 39, mkazi wa Mtaa wa Buguku, Buhongwa, anatuhumiwa kuhusika na usafirishaji haramu wa binadamu wapatao 149.

Alisema kwa mara ya kwanza polisi walifika nyumbani kwake kutaka kumkamata baada ya kupokea agizo la mahakama iliyotaka mtuhumiwa huyo akamatwe kwa tuhuma za kuficha mtoto nyumbani. Ilidaiwa mtoto huyo ni mwanafunzi.

Hata hivyo, polisi walishindwa kumkamata nyumbani kwake baada ya waumini wa mtuhumiwa huyo kutaka kuwashambulia na kuzuia wasifanye kazi yao walioagizwa na mahakama.

Kamanda Ng'anzi alisema baada ya polisi kuona vurugu hizo waliamua kuondoka na siku iliyofuata waliongeza nguvu na kufanikiwa kumkamata.

Awali Mahakama ya Mwanzo ya Mkuyuni jijini Mwanza ilitoa amri kwa Jeshi la Polisi kumkamata mzazi wa kike wa mtoto (jina tunalihifadhi) ambaye ni mwanafunzi aliyedaiwa kufichwa nyumbani kwa mtuhumiwa ili afikishwe mbele ya mahakama hiyo.

Kutokana na ukatili huo wa kuficha mwanafunzi na kusababisha ashindwe kwenda shule, mahakama iliagiza Jeshi la Polisi kwenda kumsaka mwanamke huyo pamoja na mtoto wake ambaye ni mwanafunzi.

"Siku ya kwanza askari wetu walikwenda nyumbani kwa mchungaji huyo, lakini kwa kuwa walikuwa wachache walishindwa kumkamata mchungaji na watuhumiwa wengine, hivyo askari wetu wakarudi na siku ya pili waliongeza nguvu na kufanikiwa kuwakamata watuhumiwa hao," alisema Kamanda Ng'anzi.

Alisema baada ya askari kuingia nyumbani kwa mchungaji huyo, walikuta idadi kubwa ya watu na walipofanya uchunguzi walibaini mtuhumiwa huyo alikuwa akifanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu.

Aliongeza kuwa watu hao wametolewa mikoa mbalimbali kisha mchungaji huyo kuwafungia nyumbani kwake kwa lengo la kuwatumikisha na kati yao wanaume walikuwa 57 na wanawake 92.

Kati yao, wamo watoto 24 wanaokadiriwa kuwa na umri wa kuanzia miaka minne hadi 17, ambao wamekatizwa masomo kinyume cha sheria.

Kamanda Ng'anzi aliongeza kuwa mchungaji huyo alikuwa akiwaaminisha watu hao kwamba yeye ni Mungu anayeponya, kufufua wafu na kutatua matatizo yao.

Alisema serikali ilishafuta kibali cha kuanzishwa kwa kanisa hilo na mchungaji huyo alikuwa akifanya kazi za uchungaji bila kibali.

Kifungu cha 32(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinatoa angalizo kwa mamlaka zilizomweka mtuhumiwa mahabusu ama kumfikisha mahakamani au kumtoa mahabusu ndani ya saa 24, isipokuwa kwa makosa yanayohusiana na adhabu ya kifo.


FSSP Field Support Services Project | Tanzania

**CONSULTING ASSIGNMENT**

**SUMMATIVE EVALUATION OF THE UPGRADING TEACHERS' COLLEGES (UTC) PROJECT**

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC), on behalf of our client, invites a team of eligible candidates (Evaluation Team) to indicate their interest to provide consultancy services for Summative Evaluation of the Upgrading Teachers' Colleges (UTC) Project. The project is being implemented by Ministry of Education, Science and Technology (MoEST) through a direct support from the Canadian Department of Foreign Affairs, Trade and Development (DFATD).

The Evaluation Team will be responsible for carrying out evaluation of the project in four supported Teachers' Colleges - namely Kitangali, Mpuguso, Shinyanga, and Ndala. The evaluation will be conducted in conformity with the "OECD/DAC (2010) Quality Standards for Development Evaluation" and best practices.

**The Evaluation Team is expected to comprise the following:**

a) A Lead Consultant - with at least 10 years' experience in designing and leading evaluation of international development projects.
b) Gender and Equality Expert - with at least 5 years' experience in gender equality programming; gender analysis for the social sector; and evaluation of gender equality programs.
c) Human Rights Expert - with at least 5 years' experience in human rights programming; and evaluation of human rights programs.
d) Education Expert - with at least 5 years' experience in education programming, education quality improvement programming and evaluation of education quality improvement programs.
e) Environment Expert - with at least 5 years' experience in environment and climate change programming, assessments; and evaluation of social sector programs, preferably education programs.

Interested candidates may obtain detailed description of the team requirements and services by sending a request email to **procurement@fssptz.org.** Requests for further information will be received up to three working days prior to the submission deadline. Any request received later than that may not be responded to.

Interested candidates should send their proposals ONLY electronically to **procurement@fssptz.org** not later than **8th March 2022 at 23:59 hours.** Late proposals shall not be accepted for evaluation, irrespective of the circumstances.

**FSSP Manager**

216729102

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mkazo uwe kukomesha vikwazo kwa wanawake

**MAADHISHO** ya Siku ya Wanawake Duniani yameanza na yanatarajiwa kufikia kilele chake Machi 8, mwaka huu, huku Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, akiagiza uhamasishaji katika jamii ili kufanikisha maadhimisho hayo.

Waziri Gwajima anasema, yapo mengi ambayo yanataraji kujili kwenye kilele cha maadhimisho hayo, ikiwamo taarifa ya utekelezaji wa ulingo wa Beijing, kuimarisha zaidi hamasa na kuleta usawa wa kijinsia.

Itakumbukwa kuwa ulingo wa Beijing kwa maneno mengine Mkutabo wa Nne wa Dunia wa Wanawake uliofanyika jijini Beijing, China mwaka 1995, ndio ulioweka msingi imara katika jitihada za wanawake kudai haki zao, ikiwamo kutaka usawa kati yao na wanaume.

Baada ya mkutano huo, nchi nyingi duniani zilianza kutekeleza maazimio ya mkutano huo ya kupunguza vikwazo dhidi ya wanawake pamoja na kuleta usawa wa kijinsia, hususani suala la kuweka usawa katika vyombo vya uamuzi.

Usawa wa kijinsia ni miongoni mwa mambo makubwa ambayo wanawake wameendelea kupigania kwa lengo la kutaka kuwe na uwiano kati ya wanaume na wanawake kwenye suala la uongozi.

Wanapoelekea kwenye kilele cha maadhimisho hayo, tuwashauri kuondolewa kwa vikwazo vyote ambavyo vimekuwa vikichangia kuwafanya waendelee kubaki nyuma na kusababisha kuwapo kwa malalamiko. Lakini tunaendelea kushuhudia jinsi gani serikali ya Tanzania imeonyesha utashi wa kisiasa katika utekelezaji wa maazimio ya Beijing pamoja na mikataba mbalimbali iliyoridhia hususan ya kikanda ya kuleta usawa kati ya wanaume na wanawake.

Mikataba na itifaki zilizoridhiwa na kutekelezwa kama za Umoja wa Afrika (AU) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) baada ya Mkutano wa Beijing tunaridhishwa jinsi Tanzania inavyoitekeleza. Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akijitahidi kuhakikisha anamwinua mwanamke kwa kuwateua wengi katika nafasi mbalimbali za uongozi tangu aingie madarakani takribani mwaka mmoja uliopita.

Hatua hiyo inaonyesha ni jinsi gani Rais amedhamiria kumwinua mwanamke ili asiendelee kuwa mnyonge bali afanye kazi kama mwanaume, kutokana na ukweli kwamba, uongozi si mzigo bali na akili na uwezo wa kuongoza.

Kwa mantiki hiyo, tunawashauri wanawake ambao tayari wamepata nafasi za uongozi, watekeleze majukumu yao kikamilifu ili kujijengea sifa za kuwawezesha kuteuliwe katika ngazi nyingine za juu zaidi.

Tunaamini kwamba, uongozi si kwa kundi fulani au jinsi fulani bali awe mwanaume au mwanamke anaweza kuongoza ili mradi awe na sifa na vigezo vinavyotakiwa, hivyo suala la usawa wa kijinsia haliepukiki.

Kwenye suala hili la usawa wa kijinsia, tunadhani ni wakati sasa kwa watunga sera na wale walioko katika ngazi za maamuzi kuondoa vikwazo vyote ambavyo vimekuwa vikimfanya mwanamke kubaki nyuma.

Tunashauri hivyo kwani vikwazo kwa wanawake haviko katika uongozi tu, bali hata kwenye mikopo ya halmashauri nako kuna sintofahamu inayotokana na tuhuma za baadhi ya watumishi kujineemesha na kuacha walengwa. Ikumbukwe kuwa wanawake ndiyo wanaobeba majukumu makubwa nyumbani kuanzia kwenye kulisha familia, hivyo tunadhani ingependeza kama wigo wa utoaji wa mikopo utapanuliwa na kuongeza fursa zaidi za kukopa bila riba au kwa riba ndogo.


Lakini kwenye suala la nishati, wanabeba mizigo mikubwa ya kuni kwa ajili ya kupikia nyumbani, hivyo tunashauri hata gharama ya gesi ishushwe ili wengi zaidi waweze kutumia nishati hiyo majumbani badala ya kusaka kuni na kuchangia uharibifu wa mazingira.

Iwapo hayo na mengine ambayo hatukuyataja na yamekuwa yakilalamikiwa na wanawake yakitekelezwa, dhana nzima ya Rais ya kutaka kumnyanyua mwanamke kuanzia msomi na asiye msomi, tunadhani itakuwa imetimia. Kaulimbiu ya maadhimisho hayo ya mwaka huu inasema; 'Kizazi cha Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu; Tujitokeze Kuhesabiwa', inaonyesha maendeleo endelevu yanaletwa na jinsi zote.

Watunga sera na walio katika ngazi za maamuzi, tunawashauri waangalie jinsi ya kuondoa vikwazo vinavyowabagua wanawake katika uongozi, ili kuharakisha nchini kuwa na maendeleo endelevu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Watendaji msaidieni Rais kwa kuwajibikia ya kwenu

**KWA** miaka ya hivi karibuni, kumekuwapo na taarifa nyingi za matukio ambayo wananchi wakipata matatizo, kimbilio pekee inakuwa 'Rais tusaidie.'

Matatizo mengine ni ya kawaida tu yanayoweza kutatuliwa kwa ngazi ya familia, kijiji, kata, wilaya, au mkoa, lakini utawasikia wananchi hao wakielekeza kilio apelekewe Rais wa Nchi.

Utakuta migogoro ya ardhi, wananchi wanamlilia Rais, mjane kadhulumiwa nyumba naye kilio chake kinapelekwa huko, watu wawili wameuziwa shamba moja, nao wanalalamikia hukohuko kutaka haki yao, ili mradi tu, hadi unashangaa!

Mimi ninavyojua Rais wa nchi siyo mfalme, anayeamua hata kesi za au mashauri ya kawaida.

Tanzania ina mifumo yake iliyowekwa tangu wakati wa Uhuru, wapo mawaziri, wakuu na mikoa, wabunge na wakuu wa wilaya. Nchi hii ina viongozi hata wa kata, vijiji na mitaa. Waliwekwa kwa makusudi, kuhudumia yanayofanana na upeo huo na mengine mengi. Kazi yao kubwa ni kutumikia wananchi. Pia, wanawaweka viongozi kwenye nafasi zao wawatumikie, iwe wameteuliwa au wamechaguliwa na wananchi wenyewe. Rais yeye anawategemea hao kutatua matatizo na kero za wananchi waliko. Haijulikani ni kwa nini kwa sasa mambo haya yanajitokeza, tofauti na huko nyuma.

Kwanini hayo yote? Nadhani kuna shida mahali fulani, watendaji wengi hawawajibikii majukumu yao. Au wananchi hawawaamini kiasi cha kilio chao wanataka moja kwa moja kisikike kwa Rais.

Mimi binfasi nadhani huenda kumekuwapo na kutoaminika kwa baadhi ya watendaji kwa wananchi, labda kutokana na uamuzi wao ambao wamekuwa wakiamua, kiasi kwamba wakuwa n imani haba kwao.

Pia nafikiri kumekuwapo na uzembe, au udhaifu wa kufuatilia masuala mbalimbali au matatizo mbalimbali yanayohusu wananchi na kuyatatua, tena kwa wakati muafaka. Labda ni kutokana na woga kutojiamini, na wakadhani tatizo litaisha lenyewe, lakini kumbe linazidi kujilimbikiza hadi leo likizaa hali hiyo inayoliliwa.

Jambo muhimu mbele yetu ni kwamba, watendaji wote kuanzia ngazi ya kijiji, kata, wilaya, mkoa na kuendelea kusimama kwenye nafasi zao kisawasawa.

Sidhani tutaendelea kusikia mtu kauziwa kiwanja na wahusika wa serikali, halafu baadaye inaonekana ameuziwa kimakosa, naye analalamika kwa Rais.

Rais ana mambo mengi makubwa ya kufanya, ikiwamo hata kusafiri nchi na nchi kuweka mazingira sawa na ushirikiano na watu wa mataifa mbalimbali duniani, ili uchumi uendelee kukua.

Sasa hili la kutaka awajibikie hata lililoko katika ngazi ya mwenyekiti wa serikali za mitaa, ni kuonyesha kuwa wakati anaendelea kupambania taifa kukuza uchumi, kuna watu hawawajibiki kwa kumsaidia kazi ziliziko ndani ya uwezo wao. Kwa maana hiyo, nadhani imefikia wakati watu waamke na kuwajibika, kila mtu kwenye nafasi yake aliyowekwa. Pia imefika wakati baadhi ya viongozi wanaohusika, pamoja na watu wa habari kuwapa elimu wananchi kuhusu itifaki. Inawezekana kabisa, ikawa wananchi wengi hawana elimu hiyo, ndiyo maana wao kila kitu wanalilia wasaidiwe na Rais.

Ni kweli, inawezekana ikaja siku Rais akawasikiliza, lakini wawe wamepitia ngazi mbalimbali na imeshindikana kabisa. Hata hivyo, wakati anatatua ni lazima atauliza huko kote tatizo hilo lilipopita ni kwa nini hakutatuliwa, au ugumu ulikuwa wapi, wakati wao wana uwezo wa kulimaliza kabla ya kufika kwake. Wananchi inabidi waelimishwe kuwa Rais ndiyo mtu wa mwisho na ndiyo ngazi ya juu zaidi nchini na kwa siku ana kazi nyingi mno kubwa anazopaswa kupitia, kuzikagua, kuzifanyia kazi kwa manufaa na nchi na wananchi wake kwa ujumla, hivyo matatizo mengine wayapeleke kwenye ngazi zinazohusika. Kwa sababu unaweza kusikia malalamiko ya wananchi, wakati mwingine hawajayapeleka kwenye ngazi yoyote ile, ila wakipata nafasi ya kukutana na vyombo vya habari wanataka moja kwa moja yasikike huko wanakotaka na yatatuliwe.

Wananchi wanapaswa wanajue mgogoro, kesi au tatizo hili kwanza likitokea, linaanza kuripotiwa wapi na kama ikishindikana lipelekwe wapi. Nadhani hii itapunguza kama si kumaliza kabisa matatizo hayo ambayo kwa miaka ya karibuni yameanza kujitokeza sana nchini.

Watendaji wafanye kazi zao walizozitaka wenyewe kwa kuomba kuchaguliwa na wananchi, au watekeleze kile ambacho wameapa na kuahidi kukitelekeza baada ya kuteuliza, ili kila mtu afanye kazi yake, pia wananchi nao wanatakiwa waelimishwe jinsi gani itifaki inafanya kazi na jinsi gani matatizo au migogoro yao, wapi kwa kuyapeleka.

# Serikali yapokea maoni, malalamiko 230,000 ya kuyafanyia kazi kwa mfumo wa kidijitali

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, amesema, tangu kuanzishwa kwa mfumo wa kielektroniki wa kupokea, kufuatilia na kushughulikia malalamiko (e-Mrejesho) kumekuwa na mwitikio chanya.

Amesema kutokana na wananchi na watumishi wa umma kuutumia mfumo huo, serikali imepokea na kushughulikia kwa wakati maoni na malalamiko 239,196 yaliyowasilishwa katika taasisi za umma.

Daudi alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati akifungua mafunzo ya matumizi na uendeshaji wa mfumo wa kutuma, kupokea na kufuatilia malalamiko, mapendekezo, maulizo na pongezi (e-Mrejesho) kwa maofisa malalamiko na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa sekretarieti za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa, wizara, wakala na idara zinazojitegemea Kanda ya Mashariki.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa mfumo huo wa kielektroniki, haikuwa rahisi kushughulikia malalamiko kwa wakati na kuwa na takwimu halisi za maoni na malalamiko yaliyofanyiwa kazi ambazo zinatumiwa na serikali kama mrejesho wa kuboresha huduma zinazotolewa kwa wananchi.

Pia alisema Ofisi ya Rais - UTUMISHI kupitia Idara ya Ukuzaji Maadili, imejipanga kuendelea kutoa mafunzo kwa maofisa malalamiko na TEHAMA katika taasisi zote za umma nchini ili kuwajengea uwezo wa kutumia vyema mfumo huo wa kielektroniki kushughulikia malalamiko yote yanayowasilishwa na wananchi na wadau kwa wakati.

Daudi aliongeza kuwa mfumo wa e-Mrejesho umesanifiwa kwa namna ambayo inaongeza uwazi, uwajibikaji na usikivu kwa watendaji serikalini kwa kuwa unawawezesha viongozi katika ngazi mbalimbali kuona na kufuatilia malalamiko au maoni yanavyoshughulikiwa.

"Endapo kutakuwa na ucheleweshwaji wa kutoa mrejesho au uzembe wa aina yoyote, mfumo unampa fursa kiongozi katika taasisi husika kuchukua hatua stahiki kwa wakati," alisema.

Pia alisema mfumo huo ni rahisi kuutumia kwa kuwa unamwezesha mtumishi na mwananchi wakati wote na popote alipo kutuma maoni au malalamiko na kupokea mrejesho kupitia tovuti au simu za kiganjani.

Awali, Mkurugenzi wa Ukuzaji Maadili, Ofisi ya Rais - UTUMISHI, Leila Mavika, alisema njia ambazo zilikuwa zikitumika kuwasilisha malalamiko awali zilisababisha changamoto mbalimbali ikiwamo ya kukosekana kwa takwimu sahihi za utunzaji wa takwimu za malalamiko ambazo hutumiwa na serikali kuboresha huduma na kufanya uamuzi.

Mavika alisema kabla ya serikali kuanzisha mfumo wa kushughulikia malalamiko kielektroniki, wananchi hawakuwa na fursa ya kupata mrejesho wa malalamiko yao kwa wakati, hivyo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) iliona ni vyema kuandaa mfumo wa kielektroniki ambao kwa kiasi kikubwa utaongeza uwajibikaji katika eneo la kushughulikia malalamiko.



Askari wa Kikosi cha Usalama Barabarani akimdhibiti dereva wa bajaj, baada ya kutofautiana wakati akitekeleza majukumu yake, katika eneo la Palestina, Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, mkoani Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Serikali yawatoa hofu wadau Bandari Dar

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewahakikishia wadau wa usafiri na usafirishaji wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam kuwa iko tayari kuhakikisha inaboresha mifumo na miundombinu yake ili kurahisisha biashara ndani na nje ya nchi, hivyo kuvutia watumiaji wengi zaidi.

Akizungumza katika kikao kilichowakutanisha wadau hao jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Uchukuzi), Gabriel Migire, alisema serikali inafuatilia kwa karibu changamoto zote zinazojitokeza katika usafirishaji ili kuhakikisha wanufaika ambao ni wafanyabiashara wa ndani na nje ya Tanzania, hawapati vikwazo na kuacha kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

"Niwahakikishie kuwa serikali inafuatilia kwa karibu changamoto zote zinazojitokeza katika matumizi ya bandari na hiyo inafanyika kwa kufanya vikao na kuchukua hatua kwa kila changamoto inayojitokeza," alisema.

Migire aliipongeza serikali ya Zambia kwa kushirikiana kwa karibu na Tanzania hasa ulipotokea mgomo wa madereva katika mpaka wa Nakonde nchini Zambia na kusababisha bidhaa kucheleweshwa kwa watumiaji.

Katibu Mkuu alichukua nafasi hiyo kuitaka Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) kubuni mifumo itakayowawezesha madereva wanaochukua mizigo bandarini kufuatilia mizigo wanayochukua bila kupata changamoto yoyote ili kupunguzia muda wa kukaa ndani ya bandari.

"TPA lazima muwe wabunifu mkajifunze kwa wenzenu bandari nyingine. Kwa bandari yetu hii mkiweka mifumo hasa kwenye kuchukua mizigo mtapunguza sana magari kukaa bandarini na mifumo hiyo itawarahisishia madereva wanapoingia wajue mizigo wanaichukua wapi na kisha kuipelekea inapotakiwa kwenda," alisisitiza.

Mwenyekti wa Chama cha Madereva Tanzania (ITDA), Adam Mwenda, aliishukuru serikali kupitia Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa kuchukua hatua stahiki na kwa wakati kipindi cha mgomo wa madereva katika mpaka wa Tanzania na Zambia.

Mwenda aliiomba serikali kufuatilia kwa karibu changamoto mbalimbali ambazo serikali mbili zimekubaliana katika kikao chao ili kufanya biashara baina ya Tanzania na nchi jirani kufanikiwa zaidi kwa kuwa wateja wakubwa wa Bandari ya Dar es Salaam ni Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC).

Serikali kupitia sekta ya uchukuzi imekuwa na mpango kazi wa kufanya vikao vinavyowahusisha wadau wote wa Bandari ya Dar es Salaam kila mwezi ili kuhakikisha bandari inakuwa na ufanisi na kukuza uchumi wa nchi.

# Wananchi wapinga uamuzi wa DC

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WAKAZI wa vijiji vya Msanga na Mitesa Halmashauri ya Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wamepinga uamuzi wa Mkuu wa Wilaya hiyo, Claudia Kitta na Kamati ya Maendeleo ya Kata kuhusu mapendekezo ya eneo la ujenzi wa shule ya sekondari.

Wamepinga ujenzi huo wa sekondari kufanyika Kata ya Mitesa katika Kijiji cha Maendeleo badala ya Msanga.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti kijijini hapo, walisema kuwa hawako tayari kuunga mkono ujenzi huo kwa sababu mapendekezo yaliyotolewa kuhusu ujenzi huo, wao kama wanakijiji hawayakubali hadi mapendekezo yao yatakaposilikizwa.

Walisema awali kuna eneo maalumu ambalo lilikuwa limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa shule hiyo ya Sekondari ya Kata ya Mitesa na wananchi walihimizwa kujitolea kufanya usafi kwenye eneo hilo kwa ajili ya kuanza ujenzi huo, lakini cha kushangaza baadaye uongozi wa kata ghafla umebadilisha eneo hilo bila sababu za msingi.

Abdulrahmani Rashidi, mkazi wa kijiji cha Msanga alisema mapendekezo yao ni kwamba shule hiyo inapaswa kujengwa katika Kijiji cha Msanga ambako ndiko itakuwa rafiki kwa watoto wanaoishi katika kata hiyo kufika shuleni kwa urahisi zaidi kuliko eneo ambalo limependekezwa na Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati ya Maendeleo ya Kata.

Alisema kuwa katika eneo ambalo wananchi wanalipendekeza kujengwa sekondari hiyo lina hekta zaidi ya 60 ukilinganisha na ambalo uongozi wa wilaya na kamati ya maendeleo ya kata wanapendekeza.

"Wananchi tunapinga mapendekezo ya maamuzi ya mkuu wa wilaya pamoja na kamati ya maendeleo ya kata, tunataka kufahamu sababu ipi ujenzi ubadilishwe kutoka kijiji cha Msanga ambako awali ndio tulikubaliana kujenga sekondari yetu, na sasa tunaambiwa sekondari itajengwa kijiji cha Maendeleo, hatuungi mkono ujenzi huu," alisema Rashidi.

Rashidi alisema wananchi walishaangusha mikorosho yao wakiamini kuwa shule itajengwa Msanga kama walivyoelekezwa awali, hivyo kuhoji kuwa inakuwaje uamuzi kubadilishwa ghafla.

Naye Fatuma Bakari, mkazi wa kijiji cha Msanga alisema kuanzia sasa hawako tayari kuunga mkono ujenzi huo kama utafanyika katika kijiji cha Maendeleo, badala yake wako tayari sekondari ikijengwa katika kijiji cha Msanga.

Rashidi alisema wananchi wanajua kwamba maamuzi ya kupeleka ujenzi wa shule katika kijiji cha Maendeleo unatokana na msukumo wa baadhi ya wanasiasa, hivyo hawatakuwa tayari kuunga mkono wala kushiriki katika jambo lololte la ujenzi huo.

Naye Juma Rashidi, mkazi wa Mitesa, alisema kijiji ambacho kinapendekezwa kujengwa kwa sekondari hiyo ni anakotoka diwani.

Akizungumzia sakata hilo, DC Kitta, alisema eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa sekondari ya kata ya Mitesa ambapo ni kijiji cha Maendeleo kwa kuwa lipo katikati ya vijiji vitano vinavyounda kata ya Mitesa, hivyo iwapo itajengwa hapo itarahisisha wanafunzi kufika shuleni kwa wepesi zaidi kuliko Msanga.

"Naagiza ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Mitesa ufanyike katika kijiji cha Maendeleo kwani kipo katikati ya vijiji vyote vinavyounda kata ya Mitesa, hivyo itarahisisha kila mwanafunzi ndani ya kata hii kufika shuleni kwa urahisi," alisema Kitta.

Kitta alisema serikali wilayani Masasi inapendekeza, ujenzi huo uwe kijiji cha Maendeleo, hivyo wananchi wote wanapaswa kuunga mkono ujenzi huo ili kufakinisha maendeleo badala ya kuendelea kuvutana.

# Wanafunzi mbaroni madai kuchoma pikipiki

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

JESHI la Polisi mkoani Singida linawashikilia wanafunzi sita wa kidato cha tano na sita wa mchepuo wa CBG katika Shule ya Sekondari Mwenge, Manispaa ya Singida kwa tuhuma za kuchoma moto pikipiki na kufyeka mahindi katika shamba la mwalimu wa shule hiyo lenye ukubwa wa ekari moja.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Rutabihirwa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Februari 24, mwaka huu, saa 5:30 usiku maeneo ya shule hiyo. Alisema wanafunzi hao walichoma moto pikipiki ya mwalimu wa shule hiyo yenye namba za usajili MC653 BFS.

ACP Rutabihirwa alisema uchunguzi wa awali ulibaini kwamba chanzo cha tukio hilo ni mwalimu huyo kumwadhibu mwanafunzi mwenzao wa kidato cha sita wa mchepuo wa CBG kwa tuhuma za kuficha simu darasani aliyokuwa akimiliki kinyume cha taratibu za shule.

Kwa mujibu wa kamanda, ilibainika kuwa mwanafunzi huyo alificha simu hiyo wakati walimu wakifanya upekuzi katika mabweni ya wanafunzi kwa lengo la kubaini ukiukwaji wa maadili na taratibu za shule ikiwamo umiliki wa simu. ACP Rutabihirwa aliweka bayana kwamba mbinu iliyotumika ni wanafunzi hao kufyeka shamba la mwalimu na kisha kuchukua pikipiki ya mwalimu iliyokuwa imeegeshwa kibarazani na kuichoma moto umbali wa mita 150 kutoka nyumba anayoishi mwalimu.

Kamanda hiyo alisema kutokana na tukio hilo, Jeshi la Polisi linawashikilia wanafunzi sita na kwa kushirikiana na Bodi ya Shule, linaendelea na uchunguzi wa tukio hilo.

ACP Rutabirwa alitumia fursa hiyo kutoa wito kwa wananchi wa mkoa wa Singida na jamii kwa ujumla kuacha kujichukulia sheria mkononi kwa kuwa kufanya hivyo ni kukiuka taratibu na sheria za nchi.



Wananchi wakijiandikisha kwa ajili kupata chanjo ya UVIKO-19, katika eneo la Feri, Magogoni, jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa kampeni iliyoendeshwa na Idara ya Afya katika Wilaya ya Ilala, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, kikiwamo Chama cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JJAD kuzalisha miche milioni 10 ya robusta

**Na Joseph Mwendapole**

KAMPUNI ya JJAD Kagera Farmers (T), imesema ina uwezo wa kuzalisha miche milioni 10 ya kahawa aina ya robusta ilmradi serikali hapo baadaye itoe fedha za kutosha kwa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB) kugharamia miche hiyo kwa kila mwaka, kwa gharama ya Sh. bilioni tano.

Hayo yalisemwa jana wilayani Biharamulo na mwakilishi wa Mkurugenzi wa Kampuni hiyo, Dk. John Mbogona, wakati akizungumza kwenye hafla ya ugawaji wa mbegu za kahawa aina ya robusta kwa wakulima wa wilaya hiyo.

Alisema kwa kuwa riba za benki zimeshuka, kampuni hiyo ina uwezo wa kukopa na kuzalisha mbegu kiasi hicho iwapo kutakuwa na uhakika kwamba serikali itachukua miche hiyo kupitia TCB.

Pia alisema ni muhimu kuangalia kikamilifu jinsi ya kumwinua mkulima kwa kuhakikisha anapata mapato yenye uwiano mzuri na bei ya soko la dunia la kahawa, ili watiwe hamasa kuendelea na uzalishaji wa zao hilo mkoani Kagera.

"Kwa kuzingatia juhudi hizi ambazo zinafanywa na uongozi wa mkoa wa Kagera, serikali kupitia Bodi ya Kahawa ambayo iko chini ya Wizara ya Kilimo, Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo na Taasisi ya Utafiti wa Kahawa (TaCRI) ambazo zinaendelea kuzalisha mbegu bora na miche bora ya robusta, tunaomba mpango uwekwe ili kuleta mapinduzi katika miaka 10 katika kahawa ya robusta," alisema.

Aidha, alishauri kuwapo na mpango wa miaka 10 wa kuendeleza kahawa ya robusta mkoani Kagera na lengo liwe la kuzalisha mbegu bora zenye tija ili zizalishe miche bora milioni 10 kwa mwaka kwa miaka 10 na zipandwe.

Pia alishauri TCB kuendelea kusajili vikundi na kampuni binafsi katika uzalishaji huo wa mbegu bora na miche bora kukidhi mahitaji mkoani Kagera na mfuko wa kuendeleza kahawa uundwe ambao utachangiwa na wadau mbalimbali wakiwamo serikali, halmashauri za wilaya, wanunuzi wakubwa wa kahawa, vyama vya msingi (AMCOS), vyama vikuu vya ushirika na Bodi ya Kahawa.

Alishauri maofisa ugani wawezeshwe ili wawasimamie kwa karibu wakulima ili wazalishe kahawa bora, yawepo mafunzo maalumu kwa wadau wote katika tasnia ya kahawa ya Robusta yenye nia, taasisi za kifedha ziwe na masharti nafuu kwa wakulima ili kuweza kutoa mitaji kwa ajili ya uwekezaji katika mashamba yao na uwepo mkakati wa makusudi kumwezesha mkulima kupata bei nzuri ya kahawa ili huyu mkulima ahamasike kuongeza uzalishaji.

Alisema matokeo ya jitihada hizo yatasababisha kuongezeka kwa kahawa inayozalishwa kutoka wastani wa tani 30,000 kwa mwaka 2021 mkoani Kagera, kufikia tani 58,750 ifikapo mwaka 2025/26 na hatimaye tani 233,750 ifikapo mwaka 2030/31 hivyo mapato ya wananchi, Taifa, Halmashauri, AMCOS, vyama vikuu ya ushirika, TCB, TaCRI yataongezeka sana.

"Tunapenda kuishukuru sana serikali kwa ubunifu huu, kwa kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania, kuweka mazingira mazuri ya ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali katika kutimiza malengo ya serikali ya kuongeza uzalishaji wa zao hili kwa tija hapa Tanzania. Pia tunaushukuru uongozi wa Mkoa wa Kagera na wa Wilaya ya Biharamulo kwa jinsi walivyo karibu nasi muda wote ili kufanikisha azma hii," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Biharamuro, Kemilembe Lwota, alishukuru kampuni ya JJAD Kagera Farmers na kuitaka iendelee kushirikiana na TCB kuzalisha miche bora ya kahawa aina ya robusta.

# CHAKUA yajitosa uhamasishaji chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Kutetea Abiria Tanzania (CHAKUA), kimejitosa kuhamasisha jamii kupata chanjo ya UVIKO-19, ambapo baadhi ya wanachama wake wanazunguka na watoa chanjo maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam.

Mkuu wa Operesheni na Elimu wa chama hicho taifa, Wilson Damo, aliliambia gazeti jana kuwa wanachama wa CHAKUA wanafanya kazi ya kutoa hamasa katika vituo vya kutolea chanjo.

"CHAKUA tunaamini kuwa kila Mtanzania ni abiria, hivyo ni mdau wetu ambaye tunaona ipo haja ya kumhamasiaha ajitokeze kuchwanja, ndiyo maana tukaomba serikali hasa upande wa afya tushiriki kampeni hizi," alisema Damo.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo wanachama wao wanashiriki kuhamasisha chanjo ni Feri, Coco Beach na mengine yenye mkusanyiko wa watu wengi yakiwamo ya Buguruni.

"Kaulimbiu yetu ni 'Kuchanja ni Ujanja', kwa maana hiyo ili kulinda afya dhidi ya ugonjwa huo, ujanja ni kuchanja tu, nasi tunawahimiza Watanzania ambao kimsingi sisi ni watetezi wao, waachane na elimu potofu wachanje," alisema.

Alisema wao si wataalamu wa afya, bali kazi yao ni kutoa hamasa ili watu wajitokeze kwa wingi kupata elimu na kuachana na upotoshaji, kisha waamue kuchukua hatua za kupata chanjo.

Alisema suala la chanjo limegubikwa na sintofahamu baada ya kujitokeza baadhi ya watu wanaopotosha ukweli na kusababisha jamii kuwa na hofu, na kwamba hofu inatakiwa kuondolewa kwa kupata elimu sahihi.

"Sisi tumeomba kushirikiana na watu wa afya kwa kuchangia katika uhamasishaji na kutoa elimu sahihi, ili Watanzania kwa hiari yao waamue kuchanja na siyo kukaa na hofu moyoni," alisema.

Damo alisema, chama hicho pia kinashiriki kampeni hizo nchi nzima kikiwa na wanachama ambao kila siku wanakwenda katika vituo vya mabasi na kuhamasisha chanjo na mwongozo wa kujikinga na ugonjwa huo.

"Abiria wanapata elimu kuhusu haki zao wanapokuwa katika vyombo vya usafiri, lakini wanaelimishwa na kuhamasishwa kuchukua hatua za kuchanja ili kujikinga na ugonjwa huo.

## Usanifu Uwanja wa Ndege wa Kigoma waanza

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanza usanifu wa barabara ya kuruka na kutua ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kutoka mita 1,800 zilizoko hivi sasa hadi mita 3,000 ili kuwezesha ndege kubwa kama vile Bombadier Q400 na Boeing kutua bila matatizo.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi (Sekta ya Ujenzi), Mhandisi Godfrey Kasekenya, alisema hayo juzi mkoani Kigoma akiwa katika ziara yake ya kikazi kukagua utekelezaji wa miradi ya kimkakati inayoendelea.

"Tunategemea uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kigoma uanze mwaka huu wa fedha 2021/22. Hadi sasa tuko katika hatua ya ununuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi," alisema.

Pia alisema kazi zingine zitazofanyika katika kiwanja hicho ni ujenzi wa jengo la abiria, njia za ndege, sehemu ya maegesho ya ndege, mnara wa kuongozea ndege, jengo la zimamoto, barabara za kuingia na kutoka uwanja wa ndege na taa za kuongozea ndege wakati wa usiku. Aliongeza kuwa lengo kuu la serikali ni kufanya kiwanja hicho kifanye kazi kwa saa 24.

"Lengo kubwa la serikali ni kuifungua mkoa wa Kigoma kwa njia ya anga, barabara, reli na maji," alisisitiza Mhandisi Kasekenya.

Katika hatua nyingine, Naibu Waziri Kasekenya alikagua ujenzi wa barabara ya Uvinza – Malagarasi (kilomita 51.1) kwa kiwango cha lami na kusisitiza kuwa makandarasi waongeze vifaa, wafanyakazi na kupanga mpango kazi mpya wa kutekeleza miradi hiyo usiku na mchana.

"Barabara hizi tukizikamilisha tutakuwa tumemaliza changamoto ya vumbi kuanzia Kigoma, Uvinza, Urambo, Tabora hadi Manyoni na kuelekea hadi mji wa serikali wa Dodoma," alisema.

Naye Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS) Mkoa wa Kigoma, Narcis Choma, alisema ujenzi wa barabara ya Uvinza - Malagarasi kwa kiwango cha lami unagharimu Sh. bilioni 62 na utekelezaji wake ni miezi 24.

Kukamilika kwa miradi hiyo ya kimkakati katika mkoa wa Kigoma ni moja ya azma ya serikali katika kufungua mkoa huo ambao ndio lango kuu la biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Burundi na Rwanda.

# Ndalichako aridhishwa utendaji wa OSHA

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, amesema katika kipindi cha miaka mitatu Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) imepata mafanikio kwa kuongeza idadi ya maeneo ya kazi yaliyosajiliwa na taasisi hiyo kutoka 4,003 hadi 23, 239 pamoja na idadi ya kaguzi za Usalama na Afya mahali pa kazi kutoka 96,000 hadi 784,000.

Prof. Ndalichako ameitoa kauli hiyo jana wakati akizindua Bodi mpya ya OSHA itakayohudumu kwa kipindi cha miaka mitatu, huku akiitaka kuisimamia taasisi hiyo ipasavyo ili iweze kupata mafanikio zaidi ya ambayo yamepatikana katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita.

Akizungumza baada ya uzinduzi huo, aliitaka Bodi hiyo kuwa na maono ya mbali katika kusimamia utekelezaji wa malengo ya taasisi hiyo.

Alisisitiza kuwa malengo ya serikali ni kuifikisha Tanzania katika uchumi wa kati wa juu kutoka katika uchumi wa kati wa chini wa sasa ambapo alisema ili kufanikisha azma hiyo ni lazima kuhakikisha maeneo ya kazi yanakuwa salama na rasilimali watu yenye afya njema.

"Nadhani sote tunaona jinsi Rais wetu anavyofanya jitihada mbalimbali zinazolenga kuvutia uwekezaji mkubwa ndani ya nchi yetu ili kukuza uchumi ambapo kupitia uwekezaji huo ajira nyingi zitazalishwa na ili kuwepo na uzalishaji endelevu tunahitaji watu wenye afya njema pamoja na mazingira salama ya kufanyia kazi na hapo ndipo mchango wenu unapohitajika," alisema Prof. Ndalichako.

Aidha, aliwaeleza wajumbe hao wa bodi mpya baadhi ya majukumu yao ya msingi ikiwemo kushauri kuhusu uhuishaji wa Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali endapo inakuwa imepitwa na wakati sambamba na kufuatilia mwenendo mzima wa taasisi husika kwa kipindi chote cha miaka mitano ambacho bodi hiyo itahudumu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye aliambatana na Waziri Ndalichako katika uzinduzi huo, Prof. Jamal Katundu aliwapongeza wajumbe kwa kuaminiwa na kuteuliwa na kuwaomba kufanya kazi kwa umahiri katika kuisimamia OSHA.

"Ninapohitimisha salamu zangu kwenu naomba niwaachie changamoto moja ambayo ni kufikiria kuacha alama katika Taasisi ya OSHA pindi muda wenu utakapokwisha," alisema Prof. Katundu. Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, ambaye kwa mujibu wa muundo wa Bodi hiyo ndiye Katibu wa chombo hicho, alisema bodi hizo zimekuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya taasisi anayoiongoza na hivyo kupitia bodi hiyo iliyozinduliwa taasisi yake itaendelea kukua na kupata mafanikio zaidi.

Akitoa shukrani kwa niaba ya wajumbe wenzake, Mwenyekiti wa Bodi ambaye ameteuliwa kwa kipindi cha pili kuiongoza Bodi hiyo, Dk. Adelhelm Meru, alisema yeye pamoja na wajumbe wenzake wana ari kubwa hivyo watajituma katika kutekeleza majukumu yao pamoja na kuzingatia weledi.

Aidha, baada ya tukio hilo la uzinduzi wajumbe wametembelea moja ya mashamba ya mbegu za mboga mboga na matunda ambayo ni miongoni mwa maeneo ya kazi yanayosimamiwa na OSHA ambapo mwakilishi wa Kampuni hiyo ya Enza Zaden Africa Ltd iliyotembelewa, Gerald Matowo, alieleza kufurahishwa kwao na ziara hiyo ya viongozi wa Wizara, Bodi pamoja na watendaji wa OSHA.




Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mafunzo kwa wadau mbalimbali wa utalii, wakiwamo watoa huduma za utalii kuhusu mwongozo wa kukabiliana na UVIKO-19 katika sekta hiyo, mjini Iringa jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Taasisi kutoa taarifa za mkopaji kwa Kiswahili

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya kutoa taarifa za mikopo Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania Limited imetangaza kuwa taarifa za mkopaji pamoja na maelezo ya mfumo kwa watumiaji wake, zitakuwa zikipatikana kwa lugha ya Kiswahili kuanzia sasa.

Awali, taarifa hizi zilikuwa zikipatikana kwa lugha ya Kingereza tu. Lengo la Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania kufanya taarifa hizi kupatikana kwa lugha ya Kiswahili ni kufanya walengwa wake kuzisoma na kuzielewa vyema.

Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania ni taasisi inayoongoza kwa kukusanya na kuchakata taarifa zinazomtambulisha mtu binafsi au kampuni/taasisi, taarifa za mikopo ya watu binafsi, mashirika pamoja na taasisi za kifedha kutoka vyanzo mbalimbali na kuzisambaza taarifa hizo kwa wateja wake. Taarifa hizi husambazwa katika mfumo wa Ripoti ya Taarifa ya Mikopo na hutumika katika kuwezesha wakopeshaji kutathmini ustahili, tabia na historia ya ulipaji wa madeni kwa mkopaji.

Akizungumza leo jijini Dar es Salaam jana wakati wa kutangaza kupatikana kwa Ripoti za Taarifa ya Mikopo pamoja na maelezo kwa watumiaji wa mfumo wake kwa lugha ya Kiswahili, Meneja wa Taasisi hiyo, Junaid Malik, alisema: 'Leo ni hatua kubwa na muhimu kwetu kwa kuweza kutoa ripoti hizi kwa lugha ya Kiswahili. Hii inathibitisha dhamira yetu ya kuendelea kuwahudumia wateja wetu kwa huduma bora zaidi. Hatua hii itafanya ripoti hizi kueleweka vizuri na zaidi zitawafanya wakopeshaji pamoja na wakopaji kuzitumia kwa ubora zaidi."

Malik aliongeza kuwa lugha ya Kiswahili ndiyo lugha mama kwa Watanzania, na kwamba kupatikana kwa ripoti pamoja na taarifa hizi kwa lugha hiyo zitaongeza uelewa zaidi na kuwafanya wakopaji kusimamia mikopo yao na kuwa na nidhamu nzuri ya ukopaji wa fedha.

"Wakati ripoti zetu za Taarifa ya Mikopo zikiendelea kuwa rahisi kwa kuelewa na upatikanaji wake, bado zinaendelea kubaki kuwa muhimu sana kwenye kufanya maamuzi. Taarifa na ripoti hizi zinajumuisha maelezo ya mkopaji pamoja na alama za kulipa mkopo, viashiria vya uwezekano wa kulipa mkopo pamoja na taarifa za mikopo inayopatikana kutoka kampuni za mitandao ya simu za mkononi," alisema na kuongeza:

Taarifa hizi pia hutoa maelezo ya mkopo wa mtu binafsi na uwezekano wa kurejesha hata pale hali inapokuwa tofauti na matarajio. Vile vile, taarifa ya mikopo ina alama ya mkopo iliyotengenezwa kwa ubashiri na kwa kuzingatia hali na mazingira ya mfumo wa fedha wa Tanzania."

Dun & Bradstreet Credit Bureau Tanzania inasimamiwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) chini ya kanuni za 2012 (CREDIT REFERENCE BUREAU).

# Matatizo wafanyakazi TRC, TAZARA kupatiwa ufumbuzi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, amesema serikali iko katika hatua mbalimbali za kushughulikia matatizo ya watumishi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) na Mamlaka ya Reli la Tanzania na Zambia (TAZARA) ili kuongeza tija kwa taasisi hizo.

Mwakibete alisema hayo juzi alipotembelea karakana ya kutengeneza vichwa na mabehewa ya TRC mkoani Morogoro na kusisitiza kuwa serikali itaendelea kuwekeza kwenye taasisi hizo ili kurahisisha usafiri na usafirishaji nchini.

"Changamoto za kiutumishi ambazo zimekuwa zikiendelea hapa nataka niwahakikishie kuwa zitatatuliwa na mtapata mrejesho kupitia viongozi wa taasisi. Ninaamini zikishughulikiwa kwa kiasi kikubwa zitachangia mabadiliko kiutendaji," alisema Naibu Waziri.

Mwakibete pia aliwapongeza wafanyakazi wa karakana hiyo kwa kufanya kazi kwa weledi na kujituma wakiwa na lengo la kuhakikisha kazi hazisimami katika karakana hiyo.

Naibu Waziri Mwakibete pia aliwasisitiza watumishi hao kufanya ukarabati wa vichwa na mabehewa kwa kuzingatia thamani ya fedha ili uwekezaji unaofanywa ufanyike kwa makini ili kufanya viendelee kutoa huduma za uhakika na salama.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Mhandisi Albert Magandi, alisema mpaka sasa kupitia watumishi hao wamekarabati vichwa vya treni takribani 16 kwa ajili kusafirisha mizigo na abiria na vichwa saba kwa ajili ya treni za sogeza.

Naye mmoja wa watumishi wa karakana hiyo, Vedastus Lugega, alimweleza Naibu Waziri kuwa pamoja na changamoto mbalimbali zilizoko, wafanyakazi wako tayari kuendelea kuhakikisha ukarabati unafanywa kwa wakati na kuzingatia viwango ili kutoihujumu serikali.

Naibu Waziri Mwakibete alikuwa mkoani Morogoro kwa ziara ya siku moja kukagua maendeleo ya miradi ya sekta ya uchukuzi ikiwamo mradi wa ukarabati wa vichwa na mabehewa.



Wananchi wakiangalia basi la daladala lenye namba za usajili T539 DMC, linalofanya safari zake kati ya Makumbusho na Mabwepande, baada ya kupata ajali katika Barabara ya Bagamoyo, eneo la ITV, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Gwajima ahamasisha ushiriki Siku ya Wanawake

**Na Sabato Kasika**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewataka viongozi wa tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wadau wote kuhamasisha wananchi katika maeneo yao, ili wajitokeze kwa wingi katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Dk. Gwajima alitaja njia mojawapo ambayo inaweza kusaidia kuhamasisha wananchi kuwa ni kutumia vyombo vya habari kwa kuwa vina mchango mkubwa katika kufanya uhamasishaji.

Alisema hayo juzi, akiwa katika Kata ya Kipunguni kwenye ziara ya kikazi wilayani Ilala, jijini Dar es Salaam na kufafanua kuwa maadhimisho ya mwaka huu kila mkoa utafanya kivyake.

"Machi 8 ni kilele cha maadhimisho, ili yafane, ni muhimu viongozi wa tawala za mikoa, mamlaka za serikali za mitaa na wadau wote kuhamasisha wananchi katika maeneo yao, ili wajitokeze kwa wingi kushiriki katika maadhimisho hayo," alisema Dk. Gwajima.

Dk. Gwajima alisema, kaulimbiu ya maadhimisho hayo ni isemayo; 'Kizazi cha Usawa wa Kijinsia kwa Maendeleo Endelevu; Tujitokeze Kuhesabiwa', na kufafanua kuwa ina umuhimu kwa Watanzania.

"Katika maadhimisho ya mwaka huu, kutakuwa na tathmini zikiwamo kuhusu utekelezaji wa sera mbalimbali, uwezeshaji wa wanawake, utekelezaji wa ulingo wa Beijing, kuimarisha zaidi hamasa na kuleta usawa wa kijinsia na umuhimu wa kuwajibika ili kuleta usawa wa kijinsia," alisema.

Alifafanua kuwa kaulimbiu hiyo imegusa pia suala la sensa ya watu na makazi, inayotarajiwa kufanyika Agosti 22 mwaka huu, na kwamba bila kujua idadi ya watu na huduma zinazohitajika, itakuwa vigumu kwa serikali kuainisha na kupitisha huduma na afua mbalimbli na hivyo kuathiri mikakati ya maendeleo.

"Katika kuchochea uchumi, wote twende kuhesabiwa. Wanawake tumieni nafasi zenu katika jamii kuhamasisha kuhesabiwa, ili kusaidia kuchochea uchumi na maendeleo jumuishi," alisema.

Awali akimkaribisha Waziri, Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, Seleman Bishagazi, alisema kituo kimekuwa kikipambana na ukatili wa kijinsia katika ya Kipunguni na kwamba jamii imeanza kubadilika.

"Huku jamii tuliyonayo ni ile inayotoka kwenye mikoa inayokeketa, tumejitahidi kutoa elimu kwa msaada wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na wadau wengine, tumepunguza kwa kiasi kikubwa vitendo hivyo," alisema Bishagazi.

Mkurugenzi huyo alisema, juhudi za pamoja zinahitajika ikiwamo uwezeshaji ili kukomesha ukatili wa kijinsia katika jamii na kwamba vita hiyo si serikali na wadau wachache bali ni ya jamii nzima.

## DC aonya TRA kubambika kodi

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKUU wa Wilaya ya Geita, Wilson Shimo, amewataka wafanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuacha tabia ya kuwabambikizia kodi wafanyabiashara wakubwa.

Shimo alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wakubwa wa mkoani hapa kwenye ukumbi wa GEDECO ulioko katika Halmashauri ya Mji wa Geita.

Alisema hayo anayoyasema yapo na yanalalamikiwa na inabidi ayaseme mbele yao kwa sababu hili halileti afya na kama kuna watu ndani ya TRA wanafanya mambo kinyume cha utaratibu wa kuwatisha wafanyabiashara na kuwabambikizia hizo kodi, waache mara moja.

Pia alisema kitendo hicho kimewafanya wafanyabiashara wakubwa kufunga biashara na kuhamia maeneo mengine kwa sababu wananyanyaswa na wafanyakazi TRA.

Shimo alisema TRA ni taasisi ya serikali, hivyo isikwaze upande wa pili hasa kuumiza wafanyabiashara wakubwa kwa kuwabambikizia kesi na kodi bali na kuwajengea mazingira ambayo yanawatisha, hivyo kufunga biashara au kuhama maeneo ya Geita.

Naye Mkurugenzi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) Mkoa wa Geita, Ally Abdul, akizungumza na wafanyabiashara wakubwa wa mkoa wa Geita, alisema kila fursa inawezekana kwa namna yoyote na kutoka sehemu moja kwenda nyingine, hivyo cha msingi ni kuhakikisha wanafanya uchambuzi wa kina juu ya fursa husika.

Abdul alisema wanachopaswa kufanya ni kuacha kukurupuka katika suala la kuanzisha jambo pasipo kufanya utafiti wa kutosha na kwamba kila jambo linatakiwa kuchunguzwa faida na hasara kabla ya kulianzisha.

Alisema kuna aina zingine za fursa kama uwekezaji kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi kama kilimo, uvuvi na ufugaji pamoja na elimu, biashara na afya ambazo zinaweza kumnufaisha mtu lakini cha muhimu ni kufanya utafiti wa kina.

ama
ALHAMISI MACHI 3, 2022
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Ziwa Tanganyika linavyoongezeka na janga kuu kwenye ufukwe wake**




Ukurasa 13

**KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE**

Daktari mwanamke wa kwanza nchini, mwasisi MEWATA akumbukaye mengi



Ukurasa 14

**MWENYE UMRI ZAIDI MIAKA 50...**

**Vijue vigezo, masharti kwa ngozi ya mwanamke iendelee kunawiri**

AFYA

# Pembe tatu za ukatili jinsia; usalama mtoto, kanuni sahihi, vita 'dada poa'

**Na Yasmine Protace**

NDANI ya jamii kuna msamiati unaotawala katika kutafuta haki kwa tofauti kati ya wanawake na wanaume unaoitwa 'ukatili jinsia.' Lakini, inaweza kwenda mbali ikihojiwa kwa maneno au namna tofauti.

Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA), kupitia kitabu chake 'Ukatili wa kijinsia na Athari Zake' imeandaa tafsiri ya msamiati huo; ukatili wa kijinsia, ikiuelezea kwamba ni:

"Kitendo chochote kinachoweza kusababisha madhara ya mwili, kingono, kisaikolojia au mateso kwa wanajamii, ikiwa ni pamoja na kutishiwa maisha, kunyimwa uhuru, iwe hadharani au kwa kificho."




Wakati matukio hayo yanaendelea katika jamii, kuna baadhi nao wanayafumbia macho hata yakitokea mbele ya hadhira zao, badala ya kutoa taarifa mahali husika ili mtuhumiwa achukuliwe hatua.

Kuna hatua inafikiwa hata anayefanyiwa ukatili anadumu kumficha aliyemfanyia madhila hayo. Christopher Neuton, ni mdau kutoka Dawati la Jinsia na Watoto, anayesema matukio ya ukatili yanaweza kwisha endapo wanaofanyiwa ukatili watatoa taarifa katika dawati husika, mathalan polisi ili hatua stahiki zichukuliwe.

Anasema, kuanzishwa dawati hilo Polisi kunawasaidia wanaofanyiwa ukatili wa aina yoyote, kukabiliana na matukio ya aina hiyo yanapotokea, wanatoa ushirikiano ili wanaotenda ukatili wachukuliwe hatua haraka.

"Kuna watu wanafanyiwa ukatili,badala ya kutoa taarifa anakaa kimya, kukaa kimya, ndio kunasababisha matukio ya ukatili kuendelea," anasema Neuton, anayewapa angalizo wanaofanyiwa ukatili wasiharibu ushahidi.

Anafafanua, ushahidi ni nyenzo yenye manufaa kwenye kesi inayofunguliwa, huku akiwa na ushauri kwamba wazazi na walezi wanatakiwa kutoa ushirikiano pale wanapoona ukatili umefanyika kwa watoto wao.

Asia Mkini kutoka Dawati la Mkono kwa Mkono kutoka Hospital ya Rufani Mwananyamala, jijini Dar es Salaam, anaunga hoja akisema kwa asilimia 80 ya watoto wanaofikishwa kwao wanakuwa wamefanyiwa ukatili.

Kwenye mada anayoitoa kwa washiriki wa Semina za Jinsia na Maendeleo(GDSS), mjini Dar es Salaam, Asia anasema matukio ya ukatili takwimu zaonyesha wanafanyiwa watoto wadogo kwa kiwango kikubwa.

Msisitizo wake Asia ni kwamba, yeyote anayefanyiwa ukatili ndani ya Dar es Salaam au jirani, anatakiwa kufika kituoni Mkono kwa Mkono, afanyiwe uchunguzi na matibabu yanayotolewa bure.

Asia anasema, vituo vya Mkono kwa Mkono vinatoa huduma mpaka saa tisa mchana, lakini hospitali Mwananyamala, huduma hiyo inaendelea muda mrefu zaidi.

Pia, mdau huyo wa haki za kijinsia anawazungumzia wanawake wanaouza miili yao, kwamba wanapaswa faini dhidi yao kisheria iongezwe. Anafafanua: "Unakuta wanaouza miili yao wanalipa faini ya shilingi elfu tano, hiyo faini ni ndogo na inachangia wasichana kuendelea kuwa madada poa."

Mdau wa GDSS, Hassan Hamis, anaiomba serikali iweke vituo zaidi vya Mkono kwa Mkono ili kuongezea ufanisi mwenendo huo, akitoa mfano kuwapo wakazi wa vijijini wanapofanyiwa ukatili, wanakosa pa kukimbilia.

Anasema, ni hali inayowafanya waangukie mbadala wa kukaa kimya kuyafumbia matukio, hata kudumisha hali mbaya yanapotokea magumu hayo, wao wanaendelea.

**Makala hii ni kwa mujibu wa maudhui ya semina jinsia iliyofanyika hivi karibuni.**

MAZINGIRA

# Ziwa Tanganyika linavyoongezeka kina, janga kuu kwenye ufukwe

• Utalii waangukia hasara isiyotarajiwa • Mgahawa wa kipekee 'bichi' wamezwa • Mashamba shida, kwa majirani hadithi ileile



Shule iliyotelekezwa kutokana na kufurika maji ya Ziwa Tanganyika nchini Burundi. **PICHA: JARIDA LA UN**

**Na Salome Kitomari,**

**aliyekuwa Kigoma**

KUONGEZEKA kina Ziwa Tanganyika mkoani Kigoma, kuna madhara ya kumezwa na maji huduma za kijami, makazi na biashara ufukweni, biashara zilizokuwa kando ya maji zikichwa katika hali mbaya.

Kina cha Ziwa hilo kinaelezwa kuongezeka kwa mita 4.4, jambo linaloathiri shughuli za kijamii, wavuvi wanalazimika kwenda mbali kutafuta huduma, watu wanalazimika kuyahama makazi.

Ni hali inayoathiri utalii ziwani, maji yanasogea zaidi ya mita 80 ufukweni kufikia makazi na shughuli za watu zilizofanyika nje umbali mita 60.

Utalii uliovuta wengi Kigoma ni kama Ziwa Tanganyika, Hifadhi za Taifa Gombe na Mahale, pia Makumbusho ya Dk. David Livingstone, Maporomoko ya Kalambo, sehemu za matambiko na meli ya MV Liemba.

Historia inaeleza kwa miaka 50, ufukwe huo umehamwa na wengi kwa kutojua usahihi wa walikojenga na kulima hadi mwaka 2020 maji yalivyoanza kuwafikia, kukikadiriwa zaidi ya watu 300 wanaathiriwa.

Ukanda wa athari unatajwa kujumuisha biashara, huduma na miundombinu ya umma mwalo ziwani, maegesho ya mitumbwi vyote vinaharibiwa na maji, sambamba na maendeleo muhimu kama Makumbusho ya Livingstone na Bwawa la Katubuka, ambako makazi yameharibika vibaya.

**MGAHAWA WAMEZWA**

Sehemu ya waathirika ni vijana 19 waliofungua mgahawa wa kisasa umbali wa mita 30 kutoka ziwani, biashara zimeathirika kando mwa Ziwa Tanganyika, zikimezwa na maji.

Kiongozi wa kikundi hicho, Emmanuel Matiba, anaiambia Nipashe kuwa walianzisha mradi wao mwaka 2018 wajikimu kiuchumi, wao vijana wahitimu wa Chuo cha Uvuvi Kigoma (FETA).

> **Tulikuwa tunatangaza vivutio vya Ziwa Tanganyika, tulikuwa tunatangaza samaki wa mapambo ambao wanapendwa kwenye nchi za Ulaya na nyingine, wengi walikuja kuangalia samaki na kula chakula cha asili na vingine.**

Matiba anasema pia walikuwa na biashara nyingine kama za kufuga samaki, kuku na kilimo cha mboga wakiendelea kujifunza zaidi kuendesha migahawa na ujasiriamali wa kisasa, ili kujifungulia milango ya ajira.

"Mgahawa wetu ulikuwa wa kisasa ilikuwa ni sehemu pekee kivutio hasa kwa wananchi wa Kibirizi wanaokwenda kwenye mwalo wa Kibirizi kwa ajili ya shughuli za uvuvi na biashara, lakini kwa sasa hakuna tena," anaeleza.

Anajisifu mgahawa waliomiliki wanakikundi wanane, ulipata wateja wengi wageni wa aina tofauti, kiasi cha kujivunia uwapo wa fukwe hiyo, kukipatikana vyakula vya kuvutia, hata kufungua mianya ya ajira na pato kiserikali.

"Tulikuwa tunatangaza vivutio vya Ziwa Tanganyika, tulikuwa tunatangaza samaki wa mapambo ambao wanapendwa kwenye nchi za Ulaya na nyingine, wengi walikuja kuangalia samaki na kula chakula cha asili na vingine," anasema Matiba.

Anafafanua, ghalfa maji yalijaa mahali hapo Februari mwaka jana na ilifika hatua, jengo lao lilifurika na baadhi ya vifaa kama friji vikaharibika.

Matiba anasimulia ni hali iliyowapotezea ajira vijana 19, huku Manispaa ya Kigoma ikikosa tozo ilizolipa, athari pia kwa jamii na wadau waliotembelea mwalo huo.

Matiba anajipa matumaini akisema: "Tulivumilia kwa miezi kadhaa tukitarajia maji yatapungua au tukijua kuna siku maji yataondoka. Wenyeji wanasema huwa yanakuja na kuondoka.

"Tuliweka matofali ili wateja waweze kukanyaga na kuingia, lakini kuna wakati yaliongezeka na kufunika matofali na kila wakati yalizidi kujaa tukaamua kuondoka."

Anasimulia baadhi ya wateja walivumilia kwa wastani miezi miwili, wakivua viatu kuweza kufika eneo hilo kupata chakula, na baadaye wakashindwa.

"Kulingana na historia ya wakazi husika itafika wakati maji yataondoka na mradi wetu kuendelea. Tuliwekeza fedha nyingi sana na zilikuwa hazijarudi na matarajio tuliyokuwa nayo, bado tunaamini tutarudi kwenye eneo letu," aneleza kiongozi huyo.

Anafafanua kuwa baada ya janga hilo, wakahamia katika shughuli mbadala za mapato wakijielekeza kuuza viungo vya kisasa katika namna tofauti na wengine, jambo lililomletea wateja wengi sana.

Matiba anatoa rai kwa wataalamu wawasaidie wanaojenga majengo kando ya mito, ziwa na bahari waepuke hasara inayoweza kujitokeza.

Mwaka jana Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Suleimani Jafo, alitembelea eneo hilo akisema takwimu zinaonyesha kina cha maji kimeongezeka takribani mita nne.

Pia katika hilo walioathirika zaidi ni waliowekeza ufukweni, huku akiwataka wawekezaji wote kupata kibali cha mazingira, ili wasipate hasara kwa siku zijazo kama ilivyotokea.

**NINI KILITOKEA?**

Ni katika miaka miwili ya kuwapo mvua za kupindukia, zikifuatiwa na mafuriko, maporomoko ya udongo na upepo mkali, vyote vimechochea kuongezeka kupindukia kwa kiwango cha maji Ziwa Tanganyika lenye kina kirefu zaidi barani Afrika.

Ziwa Tanganyika lenye kina mita 600, mafuriko yake yanatajwa kuchangia barabara kufurika ni kwa mujibu wa Jarida la Umoja wa Mataifa toleo la Julai mwaka jana.

Jarida hilo kipengele cha mazingira linafafanua: "Kipindi cha miaka miwili ya mvua za kupindukia, zikifuatiwa na mafuriko, maporomoko ya udongo na upepo mkali, vyote vimechochea kuongezeka kupindukia kwa kiwango cha maji katika Ziwa Tanganyika."

Hapo kunafafanuliwa maeneo mengi ya huduma za umma yameathirika. Nchini Burundi ambako kuna nyanda za chini, watu wametelekeza maeneo, nyumba nyingi ujenzi wake haujakamilika na uoto wa asili umechukua nafasi yake, kulazimisha watu kukimbia.

"Iwapo hali hii itaendelea hadi mwaka 2022, uharibifu utakuwa siyo wa kawaida, na hivyo kuhitaji mpango wa kina wa kujikwamua," amesema Gabriel Hazikimana, Mkurugenzi wa Mazingira katika mamlaka ya Ziwa Tanganyika nchini Burundi.

Ziwa Tanaganyika lenye kina kirefu Barani Afrika na la pili Duniani, linagusa pia nchi za Zambia na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kote kukiathirika na kuongezeka kina cha maji.

Pia, taarifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Uhamiaji (IOM), inataja Burundi pekee ina zaidi ya wakazi 52,000 walioathiriwa na mafuriko hayo ziwani tangu Machi mwaka jana, zaidi ya nusu ya wakazi wamekimbia.

Eneo lingine linalotajwa kuathirika ni mashamba, ikiendana na hasara ya kiuchumi kwenye chakula, hasa kwa Warundi ambao zaidi ya asilimia 90 wako katika kilimo cha kujikimu.

Burundi ni kati ya nchi 20 zilizo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, pia imo katika mataifa yasiyojiandaa vya kutosha kukabiliana na majanga asili.

Hadi mwezi Mei mwaka jana, kulikuwapo wakimbizi wa ndani 127,775, kati yao asilimia 54 ni wanawake. Aidha, asilimia 85 ya wakimbizi hao ni wa ndani ni kutokana na majanga.

Kitengo cha Kukabili Majanga na Dharura Burundi, kinatajwa hakina fedha za kutosha na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kuratibu Misaada ya Dharura (OCHA), kinasema asilimia 17 tu ya maombi ya fedha za kukimu ubinadamu ndio zilitolewa mwaka jana, Dola za Marekani milioni 194.7.

"Hivi sasa watu hawana pa kwenda, hawafahamu mlo wao wa kesho utatoka wapi," anafafanua Michael Asima, Mratibu wa Masuala ya Dharura wa IOM nchini Burundi.

Mnamo Mei mwaka jana, bidhaa za mamilioni ya fedha zilizama katika bandari ndogo ya Kibirizi, baada ya mawimbi kupasua mtumbwi uliobeba mizigo kuelekea Burundi na Congo.

AFYA

## KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI...
## MJUE PROF. ESTHER MWAIKAMBO

# Daktari mwanamke wa kwanza nchini, mwasisi MEWATA akumbukaye mengi

• Leo waungana naye kupigania chanjo ya Uviko - 19

**Na Mwandishi Wetu**




Madaktari wanachama wa MEWATA wakiwa kwenye mkutano wao mjini Dodoma, wiki hii. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

NI mama anayeweka rekodi nchini, mwaka 1969 nchi ikiwa 'mbichi' na miaka minane tu ya uhuru, mwenyewe ameshakuwa daktari.

Akilinganisha alikotoka hadi leo nchi ilikofika, anaorodhesha mambo kadhaa ya kujivuna, miaka 53 iliyopita alikuwa daktari pekee mwanamke nchini, leo ni wengi hawahesabiki tena katika umri wa wanawe waliokwishafikia nao uzee, vilevile wako wajukuu.

Prof. Esther Mwaikambo, sasa anapenda kuwa mfano wa kuigwa kutoka kwa kinamama madaktari wageni. Bado anakumbuka kipindi hicho cha mwanzo wa kazi yake, watu wengi hawakumuamini kama anaweza.

Akiwa na umri wa miaka 18 ndani ya utumishi wake, akaasisi Chama Cha Madaktari Wanawake (MEWATA), aliyoamini ingehamasisha vijana kujiunga na taaluma ya udaktari. Hapo ana angalizo kwamba hadi sasa huduma tiba kwa kinamama hazikidhi mahitaji.

Daktari Mwaikambo anasema, kinamama wameamshwa na wameshaamka, mabinti wengi shule wanachukua masomo ya sayansi na kujiunga na taaluma kama yake, ndani ya kipindi cha miaka 20 iliyopita, hali anayosema inamtia moyo sana.

Anafafanua taaluma ya udaktari katika hatua ya mwanzo huonekana kuwa na magumu kwa vijana wanaoanza, lakini kadri muda unavyoenda, somo udaktari linamuingia, hata akafahamu maana ya kuwa katika taaluma hiyo.

Mkongwe huyo anasema hawezi kukiri kinamama wamefika, bali wamepiga hatua na walikofika kuna maboresho zaidi.

Anakumbusha hali iliyotawala katika Afrika Mashariki, kulikokuwapo na mtazamo hata kliniki akiwapo daktari mwanamama, imani inayokuwepo ni kuwa haitopatikana tiba sahihi. Ni jambo lililochangia kukwamisha kinamama kutumikia jumuiya zao.

"Huu umekuwa mwelekeo wa awali, lakini naamini kwa kiasi kikubwa imeshapitwa na wakati. Nakumbuka mwaka 1969 nilipokuwa daktari rasmi. Kinamama wote hawakuwa tayari kuja kwangu kutibiwa, kwa sababu hakuwahi kuona au kusikia kuhusu daktari mwanamke.

"Mara zote waliniita nesi au msaidizi. Baadaye taratibu, walianza kuelewa mwanamama naye anaweza kuwa daktari akisaidia kinamama, wengi walibadilika mawazo yao.

"Idadi ya madaktari wanawake ikaanza kuongezeka, kinamama madaktari wakaanza kukubalika kuliko kinababa, tena kinama wanajisikia vizuri kuhudumiwa na daktari mwanamke," anaeleza.

Mama huyo analirejea Shirika la Afya Duniani (WHO), katika kauli yake ikisema nusu ya madhila ya ukeketaji yamepungua kati ya mwaka 1996 kampeni dhidi yake zilipoanza na mwaka jana, hata kukawapo nafasi kubwa kwa kinamama.

Bado anakumbuka mwaka huo kampeni za kupinga ukeketaji zikianza kuna hatua bora zimefikiwa na anasema kwa maoni yake anajivuna kuna ngazi ya ushindi, akiamini tendo hilo litazidi kutokomezwa.

"Lazima nikiri nimekuwa na taaluma iliyotukuka, kufanya kazi kama daktari na Profesa wa tiba ya watoto, basi na kutumia. Sasa ninakuwa Profesa mstaafu, katika nafasi yangu ambayo nimeitumikia kwa kipindi chote.

"Mpango wangu sasa ni kuandika kitabu, hususan katika eneo la watoto na afya zao na kuendelea kuwalea madaktari vijana, napenda wanichukulie kama mfano wa kuigwa, pia kujifunza namna wanaweza kuishi katika taaluma hii. Hivyo, ni taaluma iliyotukuka kwao," anafafanua.



Daktari wa kwanza mwanamke nchini, Prof.Esther Mwaikambo.

### MEWATA VS CHANJO UVIKO

Wiki hii MEWATA ilikutana jijini Dodoma, katika Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofunguliwa na tabibu mwenzao na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu Dk. Dorothy Gwajima

Kwenye kikao hicho chenye kaulimbiu "Kuimarisha uchanjaji wa Chanjo dhidi ya UVIKO-19 miongoni mwa madaktari wanawake Tanzania," Dk. Gwajima, anawataka waielimishe jamii kuamua kwa usahihi kuhusu masuala mbalimbali ya afya, hususan ajenda kuu ya chanjo.

Rais wa MEWATA, Dk. Mary Charles anataja lengo kuu la mkutano huo ni kuhamasisha madaktari wanawake kuwa mabalozi kwa wananchi juu ya kupata chanjo ya Uviko 19, pia wanalenga mkutanoni, kutatua changamoto mbalimbali wanazokutana nazo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Dk. Gwajima anaitaka MEWATA kuweka juhudi za kukabiliana na UVIKO-19 ikihusisha wadau mbalimbali hasa wanawake, kwa kuzingatia umuhimu wa nafasi yao katika jamii, wakiwamo wataalamu wa Maendeleo ya Jamii hususan wanawake, kwamba ni muhimu sana.

Anasema MEWATA ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, itafikisha kwenye jamii kwa ufanisi zaidi katika vita vya UVIKO -19 na mengineyo.

"Ninatambua kuwa bado kuna wananchi wengi ambao bado hawajapata elimu ya kutosha ya Chanjo ya UVIKO-19 pamoja na elimu juu ya masuala mengine ya afya . Tuendelee kushirikiana na kuwafikia kwa kuwapa elimu ya kutosha kuhusu chanjo na ugonjwa wa UVIKO-19," anaeleza.

Waziri anasema mkutano umefanyika wakati muafaka, dunia ikiendeleza jitihada za kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa huo na athari zake na MEWATA yenye wataalamu wanawake, ikishirikiana na wizara anayotumikia, itaweza kufikisha ujumbe mahali sahihi.

> **Sisi kama Madaktari Wanawake Tanzania tuna jukumu kubwa la kutoa elimu kwa jamii kwa maana ya kubadilisha fikra potofu na kuwafikishia huduma bora wananchi.**

"Ninatambua kuwa bado kuna wananchi wengi ambao bado hawajapata elimu ya kutosha ya Chanjo ya Uviko - 19 pamoja na elimu juu ya masuala mengine ya afya hivyo. Tuendelee kushirikiana na kuwafikia kwa kuwapa elimu ya kutosha kuhusu chanjo na ugonjwa wa UVIKO-19,"anasema waziri.

Rais wa MEWATA, Dk. Mary Charles anataja lengo kuu la mkutano huo ni kuhamasisha madaktari wanawake kuwa mabalozi kwa wananchi juu ya kupata chanjo ya Uviko 19, pia wanalenga mkutanoni kutatua changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza majukumu yao.

Naibu Katibu Mkuu (TAMISEMI) anayeshughulikia Afya, Dk. Grace Magembe, anafafanua:"Sisi madaktari wanawake wa Tanzania, tuna jukumu kubwa la kutoa elimu kwa jamii, kwa maana ya kubadilisha fikra potofu na kuwafikishia huduma bora wananchi."

Anaitaka MEWATA kuimarisha ushirikiano na wizara anayotumikia kuielimisha jamii ifanye uamuzi sahihi wa masuala ya afya, hususan kuhamasisha upatikanaji chanjo ya UVIKO-19.

"Sisi kama Madaktari Wanawake Tanzania tuna jukumu kubwa la kutoa elimu kwa jamii kwa maana ya kubadilisha fikra potofu na kuwafikishia huduma bora wananchi," anasisitiza Naibu Katibu Mkuu, Dk. Magembe.

Makala hii ni kwa mujibu wa vyanzo mbalimbali, ikiwamo MEWATA.

AFYA

MWENYE UMRI ZAIDI MIAKA 50...

# Vijue vigezo, masharti kwa ngozi ya mwanamke iendelee kunawiri

**Na Mwandishi Wetu**

DHANA ya mwanamama kujipamba, ni hulka ambayo ina mwenendo wa asili. Inatajwa katika kundi hilo kila mwenye zaidi ya umri wa miaka 50, kuna mapendekezo mengi wataalamu duniani kote wanajaribu kutoa kuwasaidia kutunza uhalisia wao.

Hilo linampa ujasiri na kujiamini hata akajisikia vizuri mwenyewe. Ingawa asili ya muonekano wake ni moja ya viashiria muhimu vya mwanamke , kuona anafanya ni jambo la kumtia moyo zaidi.

Inaelezwa kitaalamu si lazima mama huyo kutumia pesa nyingi au kuteseka kuweka mwili wake kuwa vizuri na afya njema.

Kuna baadhi ya mambo ya msingi yanatajwa kusaidia kuonekana hivyo bila ya gharama sana. Jarida la afya ya binadamu (WebMD) la nchini Marekani, linataja maendeleo kadhaa ya kutunza, sehemu kuu ni katika ngazi ya nywele za mwanamke.

Kuna njia nyingi zinatajwa kwa wanawake wa umri zaidi ya miaka 50, ili kuboresha sura na mwonekano wao. Hapo inaanzia mbinu kusaka kuishi maisha marefu kwa kuepuka uvutaji sigara, lishe bora na mapumziko kitandani.

Wataalamu waliohojiwa na jarida WebMD, vyote huonekana kwenye mfumo wa damu kadri umri unavyosonga, huku kukirejea hali kama za kigugumizi, kizunguzungu, kupungua uzito, na kunenepa kupita kiasi, vyote vinaweza kuathiri hali ya ngozi kunawirii.

**HALI YA NGOZI**

Kuna jambo la kwanza linashauriwa si busara kiafya mwanamama akavuta sigara na wataalamu wanasema inachangia kuharibu ngozi na dalili za kukaribisha vigezo vya uzee.

Hali kadhalika, utumiaji bidhaa za tumbaku una kawaida ya kuharibu kemikali zinazoboresha ngozi kwa haraka na inakuwa vigumu kuitengeneza.

Pili, wataalamu wanasema aepuke kupigwa na jua, hasa kutoka saa 4.00 asubuhi hadi saa 8.00 mchana, hasa kipindi cha joto kali.

Ushauri hata mama hiyo akiwa njiani juani, anapaswa kuvaa kinachofunika uso kama vile kitambaa, shati la mikono mirefu na miwani ya jua.

Tatu, kutumia mafuta ya kuzuia jua kila mara: Inashauriwa mafuta maalum yenye walau asilimia saba za oksidi ya zinki na 'SPF 30' kila siku, inayotoa kinga dhidi ya jua, ambayo ni hatari kwa ngozi. Maeneo hayo yanajumuisha usoni kila baada ya saa mbili, mtu anapotoka nje.



Kinamama wakisuka, moja ya vigezo muhimu vya fahari ya nafsi zao.

> **Hata uwe mrefu kiasi gani, kuna mambo unaweza kufanya bila kuchoka kutunza nywele zako, vilevile zikiwa ni fupi unaweza kuzirekebisha ili zionekane vizuri zaidi kwako.**



Mama mwenye mvi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Nne, ni kupima ngozi kila mara, kujihami na saratani ya ngozi: Iwapo kuna mabadiliko yoyote yanayomsumbua mtu, kunashauriwa kumfuata tabibu haraka. Tano, tayarisha ngozi kavu: Ukavu wa ngozi ni ishara kubwa kwamba kuna tatizo kubwa la ukosefu wa virutubisho vinavyofanya ngozi kuwa nzuri.

Ni muhimu kutumia kiyeyushaji na isitumiwe sabuni na mafuta ya ngozi. Mtu anapaswa kushauriana na daktari iwapo kuna matatizo yoyote.

Sita, kula vizuri na kunywa maji mengi, hiyo inatajwa kuboresha afya ya ngozi.

Saba, mtu ajaribu kutumia mafuta na losheni ya kuzuia kuzeeka, mtu mwenye umri unaozidi miaka 50, marashi na dawa zingine za ndani zinaweza kusaidia kuboresha afya ya ngozi yake.

Nane mazoezi; kwa mwanamke mwenye umri wa zaidi ya miaka 50 anapaswa kufanya mazoezi mara kwa mara na mazoezi pia ni muhimu sana, kwani inamsaidia kuongeza afya na uchangamfu wake, inaua unene ambao ni moja ya sababu za kuzeeka mapema ikiungana na matatizo ya kiafya.

Mwanamke anatakiwa asile ndio anaenda kulala.La hasha! baada ya kula kunatakiwa kuwapo muda wa saa chache kabla ya kulala. Hiyo ni kwa sababu inaweza kumfanya aangukie ziada ya lishe mwilini, hata akanenepa.

**NYWELE ZIMEKAAJE?**

Katika maisha ya mwanamke, nyweke ni kila kitu. Anapopoteza nywele au kuwapo mvi, ni mabadiliko yanayohusiana na umri na hayaepukiki.

Katika saikolojia yake, nywele ni sehemu ya uzuri na kujistahi kwa mwanamke hasa akiwa na umri wa zaidi ya miaka 50 wakati nguvu zake zikipungua.

Hivyo, anahitaji kuzitunza nywele zake maalum wakati huo huo nywele za kijivu kawaida huonekana kichwani. Kimsingi, hakuna tiba ya mvi na hakuna mwanadamu anayeweza kuepuka.

Wataalamu wanasema kuwa mvi husababishwa na upungufu wa kemikali iitwayo; melanocytes' ambayo huzipa nywele rangi na uzuri wake wa asili na kung'aa na zisipokuwapo husababisha mvi.

Mtu anaweza kuzipaka rangi nyeusi au nyingine anayohitaji, lakini anakuwa hajafuta uasilia. Inatajwa kadri mwanamke anavyozeeka, ngozi yake haitaweza kutengeneza upya seli mpya haraka kama ilivyokuwa ikifanya awali.

Virutubisho katika nywele hupunguzwa wakati wa mchakato wa rangi na vinasababisha nywele kuwa katika rangi ya kijivu.

**USHUHUDA**

Aisha ni mlimbwende mkongwe mwenye siri ya urembo wake. Anasema namna ya kubadilisha mwonekano wa nywele zake ni sehemu ya uzuri wake endelevu.

Mlimbwende huyo anasimulia kwamba, mwanamke anaweza kunenepa au kutengeneza mitindo ya kipekee ya nywele inayoendana na uso wake. Binafsi hakubaliani sana kwa wanawake wenye umri mkubwa wenye utamaduni wa kukata nywele au wasichana pekee ndio wanaacha kucha na nywele ndefu.

"Hata uwe mrefu kiasi gani, kuna mambo unaweza kufanya bila kuchoka kutunza nywele zako, vilevile zikiwa ni fupi unaweza kuzirekebisha ili zionekane vizuri zaidi kwako.

"Kuna sabuni na losheni unaweza kuzipata kwenye maduka madogo na makubwa ambayo unaweza kutumia kutunza nywele zako, ili kuongeza mvuto na kung'aa, ambao ni moja ya vitu vitakavyokufanya uonekane mzuri bila kujali umri wako," anafafanua..

Yeye binafsi anatetea urembo kwamba, haijalishi umri, ila ni mwenendo wa kudumu.

Kwa mujibu wa BBC.



## Walimu wastaafu wapewa siri kukabili vikwazo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WALIMU wastaafu wametakiwa kujiunga kwenye umoja wao ili kuwasaidia kutatua vikwazo mbalimbali ikiwamo ufuatiliaji wa pensheni zao.

Mwenyekiti wa Umoja wa walimu wastaafu wa Babati (UWAWA), Sixbert Geay aliyasema hayo jana jijini hapa mara baada ya kukamilika kikao cha walimu hao kutoka mikoa ya Dodoma na Manyara.

Alisema walimu wanapaswa kujiunga na umoja huo na kujiwekea mikakati ili kuwapo nchi nzima.

"Umoja huu ni wa msingi sana kama walimu wastaafu watajiunga wengi utaimarika na kusaidia kudai haki za msingi kwa wastaafu," alisema Gea.

Alisema lengo lao ni kuona walimu wastaafu wanakuwa na chombo cha kuwasemea kupata stahiki zao bila ya bugudha pale wanapokuwa na madai yao ya msingi baada ya kustaafu.

Kwa upande wake, Katibu wa Umoja huo, Rasuli Mshana, alisema umoja huo una mchango mkubwa kwa walimu wastaafu hivyo ni vyema kutambua umuhimu na kujiunga.

Alisema awali wakiwa kazini walikuwa na chombo cha kuwasemea shida zao, hivi sasa baada ya kustaafu nao wanapaswa kuwa katika umoja ambaoutawasaidia kujadili mambo yao yanayohusu haki zao za msingi.

"Walimu wastaafu tunatakiwa kukaa pamoja ili tuweze kushirikiana katika mambo mbalimbali ikiwamo kufuatilia haki zao, kuna walimu tangu wastaafu bado hawajapata nauli za kurudishwa makwao," alisema Mshana.

Naye Mwalimu mstaafu James Ngewe kutoka Dodoma, alisema wamejifunza mambo mengi kutoka kwa wenzao wa Babati, hivyo nao wana kila sababu ya kuiga mfano wa walimu wenzao kwa kuwa na umoja imara.

# Unyanyapaa watajwa vifo vya watu wenye Ukimwi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), imesema baadhi ya watu wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi (VVU), hufariki mapema kutokana na kunyanyapaliwa au kubaguliwa na jamii.

Kutokana na hali hiyo, inatarajiwa kuandaa mpango madhubuti wa mwaka mmoja unaolenga kuondoa ubaguzi na unyanyapaa kwa jamii.

Akizungumza juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ubaguzi Duniani hasa kwa makundi hayo, Mwakilishi kutoka TACAIDS, Jumanne Isango, alisema takwimu za TACAIDS za mwaka 2013 zinaonyesha asilimia 28 ya unyanyapaa miongoni mwa jamii.

"Watu 28 kati ya 100, wanaonyesha vitendo vya unyanyapaa dhidi ya watu wanaoishi na VVU au kuwabagua watu wanaoishi VVU," alisema.

Alisema wamekuwa wakifanya mikakati mingi kudhibiti hali hiyo kwa jamii kupitia mipango waliyojiwekea.

"Kuna matamko mbalimbali yanazungumziwa masuala ya unyanyapaa, kuna azimio la kisiasa lililotolewa kutokana na ubaguzi na unyanyapaa kuonekana ni kikwazo katika kufikia malengo tuliyojiwekea ya udhibiti Ukimwi, tunalenga kupunguza au kumaliza kabisa vifo vinavyotokana na Ukimwi kwa kuimarisha huduma mbalimbali," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa mwaka jana kulikuwa na asilimia 5.3 (watu sita kati ya 100) wanaonyesha vitendo vya ubaguzi kwa makundi hayo huku akisema lengo ni kufikia asilimia sifuri ili kuwa na jamii yenye utu na heshima.

Alisema zimekuwa zikifanyika kampeni kupitia matukio mbalimbali na kufanya makongamano ili kukabiliana na hali hiyo.

"Tuna mpango madhubuti wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na kampeni kuanzia mwezi huu hadi mwezi Machi mwakani itaenda sambamba na utekelezaji wa shughuli mbalimbali zinazolenga kuondoa suala la ubaguzi na unyanyapaa kwa makundi mbalimbali ya jamii,"alisema.

Naye mgeni rasmi katika siku hiyo, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Ummy Nderiananga, alikemea vikali tabia ya baadhi ya watu kuwanyanyapaa na kuwabagua watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi na watu wenye ulemavu.

Alisema kunyanyapaliwa kwa makundi hayo inawaathiri zaidi kisaikolojia na kukata tamaa ya kuishi.

Aidha, alisema serikali ipo tayari kufanyia marekebisho sheria na sera ambazo zimekuwa kikwazo cha kufikia malengo ya kuondokana na unyanyapaa.

"Tunapoongelea usawa wa kijinsia, mila na desturi hatarishi zinawaathiri wanawake, wasichana na watu wenye ulemavu, lakini kutokana na mila hizo imesababisha wengine kukataliwa na kutengwa na familia pindi wanapopata maambuzi ya VVU," alisema.

Awali Ofisa Programu kutoka Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na masuala ya Ukimwi (UNAIDS), Dk. Grace mallya, alisema kuwa baadhi ya mila, desturi, sera na sheria zinachangia kwa kiasi kikubwa kwa makundi mbalimbali hasa wanawake, wasichana wa rika balehe, watu wenye ulemavu na makundi maalumu kutengwa.

Naye mmoja wa watu wanaoishi na VVU, Abdul Mohamed, alisema amepitia vikwazo vingi vya ubaguzi na unyanyapaa ambapo ndugu na familia aliyokuwa akiishi nayo haikumpa huduma stahiki baada ya kuweka wazi hali yake.

"Mwaka 2014 nilikuwa namaliza elimu ya msingi ndio niliwekwa wazi hali ya maambukizi ya VVU, lakini ndugu hawakuweza kuishi na mimi, ni marehemu babu yangu ndio alinipa huduma zote lakini kwa ndugu zangu nilitengwa, nguo zangu zilifuliwa na mtu mwingine, hata vyombo vya chakula niliwekewa vyangu, nilikosa mtu wa kucheza naye, ilisababisha kwa mwaka mmoja nikaacha dawa niliumwa sana hii ilitokana na wao kunitenga na kukosa mahitaji ya msingi," alisema.




Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akizungumza na waandishi wa habari, jijini humo jana, kuhusu kampeni ya 'Ulipo Twaja' ya kuelimisha jamii suala la kupiga vita rushwa. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# N/Waziri aitaka VETA kushirikisha wananchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, ameitaka Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA), kushirikisha wananchi kwenye uandaaji wa kozi mbalimbali ili ziwe na tija kwenye maeneo yao.

Kipanga aliyasema alipokuwa akikagua ujenzi wa vyuo hivyo kwenye wilaya za Chemba na Bahi mkoani hapa ambavyo vinavyojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 2.2 kwa kila kimoja.

Alisema vyuo hivyo ni miongoni mwa 25 ambavyo vinajengwa na mamlaka hiyo kwenye wilaya mbalimbali nchini na kwamba serikali imedhamiria kushusha masuala ya ufundi kwenye maeneo hayo.

"Tunaleta Chuo cha VETA hapa, lakini wanaojua mazingira ya VETA ni hawa wananchi kwa hiyo hata kozi zitakazotakiwa hapa ni wao wanazifahamu wanajua kozi hizi zikitolewa tutatoka hapa tulipo, uanzishaji wa kozi ufanyike kikao cha pamoja nendeni kwenye mabaraza ya madiwani mpokee mawazo yao kuhusu kozi bora zitakazosaidia," alisema.

Pia alisema ujenzi wa vyuo hivyo unafanyika katika halmashauri na wilaya ambapo kuna viongozi kwenye maeneo hayo na hivyo ni muhimu wakashirikishwa katika kila hatua.

Alitaka suala la uchambuzi wa kozi zitakazotolewa na vyuo hivyo wasiutoe wao wenyewe kwenye ofisi za makao makuu yao bali wawashirikishi watu wa maeneo husika ili kukidhi maeneo husika.

"Sera yetu sasa ni kujenga chuo kimoja angalau kila wilaya na tulianza na wilaya 29 ambapo wilaya nne vyuo vimekamilika, na vingine 25 vinajengwa na VETA kwa mfumo wa 'force account' ambapo awali zilitolewa Sh.bilioni 40 ilikuwa wastani wa Sh. bilioni 1.6 kwa kila chuo, lakini ukamilishaji wa vyuo ulikuwa changamoto kidogo, awamu ya pili katika fedha tulizopata za UVIKO-19, ametoa Sh. bilioni 20 kwa ajili ya kumalizia vyuo hivi 25 na zimetolewa Sh. bilioni nane kwa ajili ya kununua samani," alisema.

Kipanga alisema dhamira ya sera ya serikali ifikapo mwezi Juni mwaka huu, uanze usajili wa wanafunzi kwa Chuo cha Chemba.

Kwa upande wao, Mkuu Wilaya za Chemba, Simon Chacha na Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Mwanahamisi Munkunda, walisema watahakikisha dhamira ya serikali inafikiwa kwenye ujenzi wa vyuo hivyo.

Naye Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo, alisema vyuo hivyo vina uwezo mkubwa wa kubadilisha maisha ya watu na kwamba bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha kunakuwa na wahitimu wengi wa vyuo vya ufundi kuliko wale wa shahada.

Awali, Mkuu wa Chuo cha VETA mkoani Dodoma, Stanslaus Ntibara, alisema wanafunzi 300 watadahiliwa kwenye fani sita za muda mrefu baada ya kukamilika kwa ujenzi huo huku kwa mafunzo ya muda mrefu wanakadiria wanafunzi kati ya 250 hadi 400 kudahiliwa kwa mwaka.





# Bodi NHIF yawaomba ushirikiano viongozi dini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BODI ya Wakurugenzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imewaomba viongozi wa taasisi mbalimbali zikiwamo za dini, kusaidia kutoa elimu kwa wananchi ili wajiunge na mfuko huo na kuwa na uhakika na afya zao.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Juma Muhimbi, alitoa rai hiyo juzi jijini Mbeya wakati wa kutiliana saini kati ya mfuko huo na Jumuiya ya Wamiliki na Wawekezaji katika Sekta ya Elimu (TAPIE) unaolenga kuwaunganisha wanafunzi kwenye mfuko huo.

Wanafunzi wanaotakiwa kuunganishwa na mfuko huo ni wa shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati vinavyomilikiwa na watu binafsi pamoja na taasisi za dini. Muhimbi alisema mpaka sasa ni asilimia nane tu ya Watanzania wote ndio waliojiunga na mfuko huo, hali ambayo alisema inaonyesha hamasa bado ni ndogo miongoni mwa wananchi.

Aliwaomba viongozi wa taasisi hizo kuhakikisha wanawahamasisha wananchi wakiwamo wafanyakazi wao kujiunga na mfuko huo ili kuongeza idadi ya wanufaika wa mfuko huo.

“Wote hapa tunao wajibu wa kuhamasisha wananchi ili tuongeze idadi ya wanufaika zaidi ya hii asilimia nane ya sasa, tunatakiwa tufike mahali kila Mtanzania awe mwanachama wa mfuko huu,” alisema Muhimbi.

Mkurugenzi wa NHIF, Bernard Konga, alisema kutokana na idadi hiyo ndogo ya Watanzania waliojiunga na mfuko huo, wameanza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wanaongeza idadi na ikiwezekana Watanzania wote wawe wanachama.

Alisema kwa sasa wameamua kuwekeza nguvu kubwa kwenye kundi la kati ambalo ni la vijana wa shule za msingi na sekondari ambao ni kundi kubwa na litasaidia kutoa hamasa kwa wazazi.

Alisema kwenye maeneo ya vyuo wameshafanikiwa kwa kuwaunganisha wanafunzi wengi kujiunga na mfuko huo na kwa sasa wanaendelea na ngazi za chini. “Tutaendelea kutoa taarifa ya namna tunavyoendelea kuwasajili wananchi, kwa sasa tumeanza na sekta binafsi na kumekuwa na mwitikio mzuri sana na tunawapongeza wenzetu hawa kwa mwitikio wao,” alisema Konga. Mwenyekiti wa TAPIE, Mohmoud Mringo, alisema jambo hilo siyo jipya kwao, hivyo watahakikisha wanafunzi wote wanaingia kwenye mfumo huo wa bima ya afya.

Alisema utaratibu ulioanzishwa na NHIF utawasaidia kupanua wigo wa matibabu kwa wanafunzi kwa kuwa awali walikuwa wana utaratibu wa kuhakikisha wanafunzi wao wanajiunga na mfuko huo.

Mringo alisema kuwa yeye binafsi kwa kipindi cha miaka mitano sasa hawezi kupokea mwanafunzi ambaye hajajiunga na bima ya afya na hivyo akawataka wamiliki wengine wa taasisi za elimu kuwa na mfumo huo.

Katibu wa TAPIE, Mpoka Mwambusi, alisema walikubali utaratibu wa kuunganisha wanafunzi na mfuko huo kwa sababu wana imani kuwa kundi hilo ni kubwa na ndilo taifa la kesho.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, akichangia damu katika Shule ya Sekondari ya Sangu, shughuli iliyoratibiwa na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania wilayani humo jana. Kushoto ni Mteknolojia wa Maabara ya Hospitali ya Igawilo, Dk. Jovin Rwegasira. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wavuka lengo la ukusanyaji damu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya chupa 180 za damu katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya zimekusanywa na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania katika kipindi cha mwezi Februari, mwaka huu na kuvuka lengo la ukusanyaji wa damu la chupa 167 kila mwezi.

Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo kwa Mkoa wa Mbeya, Ibrahim Bombo, alibainisha hayo jana wakati wa kuchangia damu katika Shule ya Sekondari Sangu.

Alisema lengo la kuhamisisha uchangiaji damu ni kuokoa maisha ya wanaojifungua, wanaofanyiwa operesheni na majeruhi.

Alisema uhamasishaji umesaidia kuokoa maisha ya wananchi wengine ambapo hadi sasa wamevuka lengo la asilimia 100 katika ukusanyaji damu kila mwezi kwa Jiji la Mbeya na wataendelea kuhamasisha shule nyingine ili kukusanya zaidi chupa za damu.

“Mbali na Jumuiya ya Maridhiano Tanzania kufanya shughuli za usuluhishi na utatuzi wa migogoro mbalimbali ikiwamo ya kisiasa, kidini na kiutamaduni, tumeamua kujikita pia katika kuhamasisha uchangiaji damu kwa wananchi ili kuokoa maisha ya wagonjwa walioko hospitalini,” alisema Bombo.

Akishiriki uchangiaji wa damu, Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema yeye ni miongoni mwa wadau wakubwa wa kuchangia damu mara kwa mara.

Alisema uamuzi wa jumuiya hiyo kuhamisisha uchangiaji damu ni upendo wa hali ya juu na serikali itaendelea kuhamasisha wananchi kuchangia damu ili kuokoa maisha ya wahitaji.

“Niliwahi kuokoa maisha ya mjamzito ambaye alikuwa anahitaji damu B+ ili kufanyiwa operesheni na mimi ndiye mtu pekee ambaye nilikuwa na kundi hilo la damu, nilijitolea na kuokoa maisha yake na sasa tumekuwa ndugu, nawahamasisha wenzangu tuchangie damu ili tuwasaidie wenzetu huko hospitalini,” alisema Dk. Chuachua.

Miongoni mwa wanafunzi waliochangia damu kutoka Sekondari ya Sangu, Kelvin Alex, alisema alihamasika kuchangia damu baada ya kuona hali za wagonjwa hospitalini.

Aliipongeza Jumuiya ya Maridhiano kuhamasisha wanafunzi wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea ili kuchangia damu.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Sangu, Ismail Mungure, alisema ataendelea kuhamasisha wananchi wake kuchangia damu na utaratibu huo kwake utakuwa endelevu.

## Mil. 60/- zahitajika ujenzi uzio shuleni

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

ZAIDI ya Sh. milioni 60 zinahitajika kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa Shule Jumuishi ya Msingi Katumba II iliyoko wilayani Rungwe mkoani Mbeya, ili kuepusha watoto wenye ugonjwa wa akili kutoroka shuleni mara kwa mara.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney, aliyasema hayo juzi alipokabidhi mradi wa ufugaji wa nguruwe na kuku kwa vikundi vya watu wenye ulemavu waliotambuliwa na kusaidiwa na Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini.

Dk. Anney aliwaomba wadau mbalimbali wa maendeleo wa wilaya hiyo kushirikiana na serikali kujenga uzio huo ili kuondokana na tatizo hilo la wanafunzi hasa wenye tatizo la mtindio wa ubongo kutoka nje ya shule wakati wa masomo.

Alisema shule hiyo inatoa huduma kwa wanafunzi wa mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na hivyo inahitajika kuboreshewa miundombinu yake ili wanafunzi hao wasome katika mazingira rafiki kulinga na hali zao kiafya.

“Vilevile, tunatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni matatu ya kulala wanafunzi hawa, nawaomba pia ninyi watu wa kanisa mtusaidie pia kwenye hili pamoja na wadau wengine ili watoto wetu hawa wawe salama,” alisema Dk. Anney.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Kanisa la Moravian Tanzania Jimbo la Kusini, Mch. Yona Mwambeta, alisema kanisa hilo liko tayari kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu inayohitajika shuleni huko.

Alisema tayari kanisa hilo limetenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule katika wilaya hiyo na hivyo wanasubiri wapelekewe vipaumbele vya halmashauri ili wazielekeze fedha hizo kwenye miradi husika.

“Tupo tayari kushirikiana na wilaya yako na tayari tumetenga fedha kwa ajili ya miundombinu hasa ya kuwasaidia watoto wenye ulemavu, tunakuahidi kuwa tutaendelea kushirikiana na wewe,” alisema Mwambeta.

Askofu wa Kanisa hilo Jimbo la Kusini, Kenani Panja, alisema kanisa hilo litaendelea kushirikiana na serikali kwenye utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo na hivyo akaomba wapewe taarifa mara kwa mara.



## Zanzibar yakumbushwa maendeleo ya uwekezaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imetakiwa kutekeleza mpango wa maendeleo kwa mwaka 2022-2023 kwa kuyatangaza zaidi maeneo huru ya kiuchumi yaliyo Micheweni Pemba.

Kwa kufanya hivyo, amesema kutawezesha wawekezaji kuwekeza katika kisiwa hicho, hatua ambayo itafunguwa fursa za kiuchumi na uwekezaji.

Hayo yalisemwa na Mwakilishi wa Micheweni, Shamata Shaame Khamis, wakati akichangia mwelekeo wa mapendekezo ya mpango wa maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022-2023 katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani Unguja.

Alisema serikali ya Zanzibar imeyatangaza maeneo huru ya kiuchumi yaliyoko Fumba na Micheweni tangu mwaka 1992 lakini kwa hakuna juhudi za kuyaendeleza kwa upande wa Pemba.

Shamata alisema mpango wa maendeleo kwa mwaka 2022-2023 ujikite zaidi katika kuweka miundombinu muhimu ya majisafi na umeme hatua ambayo itawavutia wawekezaji.

"Mheshimiwa Naibu Spika naiomba serikali kuhakikisha maeneo huru ya uchumi yaliyotengwa huko Micheweni yanatumika kikamilifu na kuwawezesha wawekezaji kuwekeza," alisema.

Naye Mwakilishi wa Viti Maalum, Bihindi Hamad Said, alisema maeneo huru ya uwekezaji yaliyoko Micheweni kama yatatumika vizuri kuyatangaza kwa wawekezaji, yanaweza kuleta mabadiliko makubwa kiuchumi na uwekezaji.

"Mheshimiwa Naibu Spika wakati umefika maeneo huru ya kiuchumi yatumike kikamilifu kuona yanaleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na uwekezaji," alisema.

Kwa upande wake, Mwakilishi wa Ziwani, Suleiman Makame, aliitaka serikali kuanza kuwapatia zana wavuvi zitakazowawezesha kuvua katika eneo la bahari kuu na kupata kipato kikubwa cha samaki.

# Mwakilishi asema kuna kero za Muungano za kufuatiliwa zaidi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Shaurimoyo ambaye ni Mnadhimu wa Baraza la Wawakilishi kutoka CCM, Hamza Hassan Juma, amesema bado kuna kero za Muungano ambazo zinahitaji kufuatiliwa zaidi kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wakiwamo mawaziri wake.

Aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akichangia taarifa ya wajumbe wa baraza hilo kuhusu wabunge watano ambao huliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakiongozwa na Mwantatu Mbaraka Khamis.

Hamza alisema kimsingi kero zimepatiwa ufumbuzi na vyombo husika, lakini tatizo kubwa liko kwa upande wa watendaji wanaofanya kazi katika sehemu za bandarini na uwanja wa ndege.

"Mheshimiwa Naibu Spika wako wawakilishi wanaotuwakilisha bungeni ambao tunawapa kazi wafuatilie zaidi kero za Muungano zikiwamo za wafanyabiashara wetu wadogo kuona wanapiga hatua kubwa ya maendeleo na kuepukana na vikwazo vya kibiashara," alisema.

Akiwasilisha ripoti ya taarifa ya wawakilishi watano ambao huingia katika Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mwakilishi Mwantatu alisema wamekuwa wakifanya mawasiliano kwa mawaziri husika kuhusu changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika Muungano kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.

"Changamoto zote za Muungano sisi kazi yetu kuziwasilisha mbele ya bunge au kwa mawaziri husika wa taasisi za Muungano na wenzetu wamekuwa wasikivu sana,' alisema.

Wawakilishi watano wanaoliwakilisha Baraza la Wawakilishi katika Bunge la Muungano ni Mwantatu Mbarak Khamis, Bakari Hamad Bakari, Ameir Abdalla Ameir, Bahati Khamis Kombo na Suleiman Haroub Suleiman.

Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Oktoba 30, 1984 lilitunga Sheria ya Marekebisho ya tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 ambayo ilifanya marekebisho makubwa ikiwamo muundo wa Bunge la Jamhuri.

Katika marekebisho hayo, kifungu cha 13 cha sheria hiyo kilirekebisha ibara ya 66 ya katiba na kuweka idadi ya wabunge watano kutoka Baraza la Wawakilishi kuingia katika Bunge la Muungano.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walioingia bungeni kupitia nafasi tano za wawakilishi ni Rais mstaafu Dk. Salmin Amour Juma mwaka 1985-1990 na Dk. Amani Abeid Karume mwaka 1990-1995.



Mwakilishi wa Viti Maalum Mkoa wa Magharibi Unguja, Fatma Ramadhan Mandoba, akichangia hoja katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yajipanga kurejesha hadhi ya nazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imejipanga kurudisha hadhi ya minazi, zao ambalo ambalo miaka ya nyuma Zanzibar ilikuwa ikiongoza kwa usafirishaji wake na kuzalisha mafuta.

Kaimu Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Nassor Ahmed Mazrui, alisema hayo jana wakati akitoa ufafanuzi wa swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said, aliyetaka kujua mikakati ya serikali kurudisha hadhi ya zao hilo.

Mazrui alisema juhudi hizo zinahitajika kwa ajili ya kuifanya Zanzibar kuwa maarufu katika uzalishaji wa mazao ya viungo katika mwelekeo wa kibiashara zaidi.

Alisema Wizara ya Kilimo imeanza kuchukua juhudi za kuwashajihisha wakulima kuotesha miche ya minazi aina ya mbegu refu ambayo inastahamili kuishi kwa muda mrefu.

"Tumeanza kushirikiana na wenzetu wa Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo kuwashajihisha wakulima wetu kuotesha mbegu za minazi mirefu (African Tall) yenye uwezo mkubwa wa kustahamili mazingira mbalimbali ya kuishi na kuzaa kwa wingi," alisema.

Alizitaja juhudi hizo kuwa ni pamoja na maadhimisho ya siku ya upandaji miti mwaka jana ambapo zaidi ya minazi 2,000 iliooteshwa katika maeneo mbalimbali ikiwamo katika Bonde la Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Visiwa vya Zanzibar katika mwaka 1960 vilikuwa vikiongoza katika usafirishaji wa nazi pamoja na mbata katika nchi za Bara Hindi hadi Arabuni kwa ajili ya uzalishaji wa mafuta ya nazi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## TANGAZO

NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA MAKUMBUSHO KARIBU NA KITUO CHA MABASI.

WASILIANA NA 0654251570 AU 0686096001

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamiziwa mrathi Na 16/ 2022**

**Katika shauri la mirathi ya SHADRACK LAZARO KIPAGATYE.....Marehemu Wa MAKAMBAKO**

**Katika shauri la maombi ya kumteua msimamizi yaliyoletwa na TUMAINI KIPAGATYE ......Mwombaji.**

**TANGAZO KWA UMMA.**

**(Kanuniya 5(2) yakanuni za usimamizi wa Mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote /maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuudhuria katika shauri hili endapo wakita kakufanya hivyo mnamo tarehe ...21.......mwezi ...03..... mwaka... 2022..... kabla ya huyo muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpakata rehetajwa hapo juu.
**Zingatia;**Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe...18.... mwezi ...02.... Mwaka...2022

---

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**(PCA 65)**

**Kuitwa Shaurini kwa Mdaiwa**

**Mahakama ya Mwanzo ya Mjini wilaya ya Shinyanga.**

**Madai No......8/2022......**

**Mdai; Kilima Mbwiliza..**

**Dhidi ya**

**Mdaiwa..... Titus Mwita**

**Kwa; .........Titus Mwita**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba eleza habari za mdai kwa ufupi TSHS....21,500,000/=**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya Tarehe 15/03/2022 saa 2;30 Asubuhi bila ya kukosa kufika madai hayo kwa kuwa wiki hiyo ni siku ya kutajwa kwa shauri hili ni lazima uhudhurie.
Angalia kama hukuhudhuria na Mahakama ikithibitisha kuwa umepokea kuitwa shaurini kesi hii itasikilizwa bila wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo Jumanne tarehe 01/03/2022.

---

**IN THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**MOROGORO REGISTRY**
**AT MOROGORO**

**LAND REVISION NO: 21 OF 2021**

**BETWEEN**

**MARGARETH MATILDA............................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**ADAM HASSAN CHANDE, JUMA S.KACHEMELA, HARRIETH N.BANZI, NARRIS BONI SHAO, MOROGORO MUNICIPAL COUNCIL, COMMISIONER FOR LANDS, ATTORNEY GENERAL............................DEFENDANT**

**NOTICE OF MENTION**

**TO: ADAM HASSAN CHANDE, JUMA S.KACHEMELA.......DEFENDANT**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention on 24thday of March 2022 at 09:30 AM at the High Court of Tanzania at Morogoro. Your required to appear in person or through your Advocate or Agents dully authorized to appear on your behalf.

**TAKE FURTHER NOTICE THAT** in default of your appearance on that day and time the court may proceed with the application for mention in your absence.
GIVEN under my HAND and SEAL of the COURT this 17th day of February 2022.

DEPUTY REGISTRAR
MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu, **YONAH BALABALA NGASSA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari Aina ya costa Min Bus yenye namba za usajili **T 465 AMN** kwa atakae iona atoe Taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa Kumb: **MWA/NYA/RB/74059/2022.**

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO 22 OF 2022**

**In the Matter of the Estate of the Late CHARLES BORA MASNJA**

**By 1. SIMON MAGANGA MASANJA**
**2. .......................................**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 10 day of March..2022

Dated at Morogoro this 17 day of FEB..2022

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Morogoro**
**Kituo cha MJINI Mkoa Wa Morogoro**

**Usimamizi wa Mirathi......04..2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: REHEMA SIMBA MATITU WA M/MPYA KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: ASIA SIMBA MATITU**

**TANGAZO**

***(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)***

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 10/03/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 21/01/2022

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

---

## KUPOTEA KWA KADI GARI

**MOHAMEDI OMARY MSHUNGA**

Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari na plate namba (toyota hiace ) yenye namba za usajili **T 965 DND** yeyote atakae iyona atoe taarifa kituo cha polisi au piga simu namba **0712289442**

**MOR /MOR /RB/88844/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya ............TANGA**

**Kituo cha..... MJINI TANGA.... Mkoa... TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi............30............2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ROBERT DINGO ROBERT**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**

**NA: ROBERT DINGO SALIM**

**TANGAZO**

**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslai yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 9/3/2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo 16/02/2022

HAKIMU
HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
TANGA MJINI

---

## MAGARI YANAUZWA

Mazda CX7 special edition (nyeusi) 4WD 2,300 c.c petroli.
Ipo katika hali nzuri.
Imetembea 65,000km.
Toyota Cami (nyeusi) 4WD, 1,300 c.c petroli.
Ipo katika hali nzuri.
Imetembea 115,000km.

**Kwa maelezo piga 0737 708890 au 0755 378346.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BROTHERS CAPITAL INVESTMENT CO. LIMITED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 307 DQW – SCANIA. CHASSIS NO. XLEP8X40004496243. ENGINE NO. 6197169.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/OST/RB/80908/2022.**

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JESCA FRANK MLAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 508 DFE – TOYOTA RAV 4. CHASSIS NO. ZCA260071606. ENGINE NO. 1ZZ2303041.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/87594/2022.**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO....... 2022**

**In the Matter of the Estate of the late HAGARY WILSON NAMGA of ITEGA within Dodoma Region.**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY GEOFREY JOSEPH KIMARO**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

**All PERSONS claiming** to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 04 Day of 03, 2022

Date at Dodoma this **26TH day of JANUARY 2022**

PETITIONER

RESIDENT MAGISTRATE

---

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE

# Wakimbizi wafikia 870,000

• Russia yasisitiza wakazi Kyiv kuondoka



Mwanajeshi Valery (37), akiwa na mtoto akiwasaidia kuondoka na familia yake jana, kwa kutumia njia ya daraja lililoharibiwa mjini Kyiv, nchini Ukraine. **PICHA: AP**

**Kyiv,** UKRAINE

INAKADIRIWA kwa kipindi cha wiki moja idadi ya wakimbizi kutoka nchini Ukraine imefikia 875,000 tangu Russia ilipoanza kufanya mashambulizi, kwa mujibu wa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Kati yao 450,000 wameelekea nchini Poland na wengine kwenda Romania, Slovakia, Moldova na Hungary, kutafuta hifadhi.

Hapo jana, Shirika la habari la UNIAN, liliripoti kwamba shambulio la roketi huko Kharkiv, limepiga jengo la Idara ya Polisi ya Mkoa katika mji huo.

Video iliyotumwa kwenye chaneli ya Telegram ya mshauri wa serikali ya Ukraine inaonesha jengo likiteketea kwa moto. Anton Geraschenko, mshauri wa Waziri wa Mambo ya Ndani wa Ukraine, amesema jengo la Chuo Kikuu cha Kitaifa cha Karazin pia linateketea baada ya shambulio hilo.

BBC, ilidai bado haikuthibitisha video hiyo na kwamba takriban watu 21 wameuawa katika shambulizi la makombora Mkoa wa Kharkiv.

Wakati hayo yakiendelea mikutano ya kimataifa kuhusu Russia na Ukraine, imeendelea kufanyika na jana Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Kimataifa wa Nishati ya Atomiki (IAEA), Rafael Grossi, alikutana na wajumbe kadhaa kujadili usalama wa maeneo ziliko silaha za nyuklia, Ukraine.

Kadhalika, baadhi ya Waukraine wameomba Kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Francis kuzungumza na Rais Putin, kusaidia kuokoa raia wanaoathiriwa na vita hasa watoto na wanawake.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson anasema anaimani kwamba Russia inachokifanya Ukraine ni dalili ya uhalifu wa kivita.

"Tulichokiona kutoka kwenye uongozi wa Vladimir Putin ni uhalifu, kwa mtazamo wangu vita hii ina vigezo kabisa vya uhalifu wa kivita," Johnson kwenye bunge la Uingereza.

**Navalny, ambaye ni mpinzani wa muda mrefu wa Rais Putin, amekaa mwaka mmoja gerezani baada ya kunusurika shambulio la sumu ambalo anailaumu Ikulu ya Kremlin.**

### RUSSIA YADAI NI VITA YA 'KAWAIDA'

Waziri wa Mambo ya Nje wa Russia, Sergei Lavrov amesema kwamba kinachotokea Ukraine ni operesheni ya kawaida ya kijeshi na kwamba isilinganishwe na vita Kuu ta Tatu ya Dunia, kama ambavyo inadhaniwa.

"Vita Kuu ya Tatu ya Dunia, itahusisha silaha za nyuklia na za kufanya uharibifu mkubwa." Waziri huyo alinukuliwa na chombo cha habari RIA.

Lavrov anasema Russia imezindua operesheni maalumu Ukraine wiki iliyopita, huku mazungumzo ya awamu ya pili yakiendelea jana, ingawa mamlaka ya Ukraine haikuthibitisha kuendelea na mazungumzo.

Msemaji wa Ikulu ya Kremlin, Dmitry Peskov anasema kulikuwa na mkanganyiko kwenye mazungumzo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki kwa siku mbili kwenye mpaka wa Belarus-Ukraine, ambayo hata hivyo yaliishia kutokubaliana.

Peskov alisema nchi yake imekwishazoea kupitia vikwazo kadhaa na imejipanga. Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy juzi alisema kwamba Russia ni lazima isitishe mashambulizi kwenye miji mikuu ya nchi yake, kabla ya mazungumzo zaidi ya amani.

### MPINZANI WA PUTIN AITA MAANDAMANO

Kiongozi wa upinzani wa Russia aliyefungwa jela, Alexei Navalny amechapisha ujumbe kwenye mtandao wa Twitter wenye maneno makali, akitoa wito wa kufanyika kwa maandamano ya kila siku nchini Russia na kwingineko.

Navalny, ambaye ni mpinzani wa muda mrefu wa Rais Putin, amekaa mwaka mmoja gerezani baada ya kunusurika shambulio la sumu ambalo anailaumu Ikulu ya Kremlin.

Mwezi uliopita alifunguliwa mashtaka mapya ambayo yanaweza kuchangia kifungo chake kuongezwa kwa zaidi ya muongo mmoja.

"Sisi, Warussia tunataka kuwa na taifa la amani. Lakini huenda ni watu wachache wanaweza kutuita hivyo sasa," ameandika kutoka gereza lenye ulinzi mkali mashariki mwa Moscow ambako amefungwa.

"Lakini Warussia wanapaswa angalau wasiwe taifa la watu wasio na hofu ambao wanajifanya kuwa hawatambui vita," anasema Nalvany na kuongeza...

"Ni muongo wa tatu wa Karne ya 21 na tunatazama habari kuhusu watu wanaochomeka kwa mabomu, nyumba zinapigwa mabomu. Tunatazama vitisho vya kweli vya kuanzisha vita vya nyuklia kwenye televisheni zetu."

### SIKU NANE UKRAINE

Wiki moja baada ya Russia, kuvamia Ukraine, lakini kufikia sasa havijafanikiwa kuuteka mji mkuu Kyiv na miji mingine mikubwa.

Wanajeshi wa Russia, wanaotumia parachuti wametua Kharkiv mji wa pili kwa ukubwa nchini Ukraine

Wizara ya Ulinzi ya Russia, pia imedai kuteka bandari ya Kusini ya Kherson.

Russia, imewaomba wakazi kuondoka Kyiv, kabla ya kufanyika kwa shambulio la kupangwa dhidi ya jiji hilo.

Msafara wa magari ya vita ya umbali wa maili 40 umesalia Kaskazini mwa Kyiv.

Russia, ilianzisha mashambulizi yake, mapema Alhamisi wiki iliyopita kutoka pande tatu kuu, Kaskazini, Kusini na Mashariki, ardhini, majini na angani. Tangu wakati huo, wanajeshi wake wamemiminika nchini Ukraine na maeneo kadhaa yamelipuliwa kwa mizinga kutoka angani.

Wanajeshi wa Russia, wamekuwa wakielekea mjini Kyiv kutoka upande wa Kaskazini, ingawa juhudi hizo zimefifia katika kipindi cha saa 24 zilizopita.

Msafara huo wenye urefu wa maili 40 ulionaswa katika picha za satelaiti, umetatizwa na magari yaliyoharibika, kulingana na wachambuzi.

Mji mkuu, Kyiv, umekumbwa na mashambulio kadhaa kutoka angani.

Siku ya Jumanne, wanajeshi wa Russia walishambulia mnara wa televisheni mjini Kyiv, huku watano wakidaiwa kuuawa na kukatiza matangazo ya vituo kadhaa ya habari.

Uwanja wa ndege wa Hostomel, umeshhudia makabiliano makali na kudhibitiwa na pande tofauti katika siku chache zilizopita, kulingana na Taasisi ya Mafunzo ya Vita (ISW).

Vikosi vya Russia karibu na Obolon, viungani mwa Kyiv, siku ya Ijumaa, viliripotiwa Kaskazini-Magharibi mwa Kyiv mwishoni mwa wiki iliyopita.

Hadi jana, vifaru vya Russia na magari ya silaha hayajaonekana katika mji mkuu, Kyiv.

**Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao**

HABARI MICHEZO

# SHIME AKUNWA HAMASA, KUJITUMA WANAWAKE U-17

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

HAMASA kubwa pamoja kujituma katika mazoezi kunakoonyeshwa na wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, kunampa matumaini Kocha Mkuu wa kikosi hicho, Bakari Shime, ya kufanya vizuri katika mchezo wao ujao, ameeleza.

Timu hiyo imeweka kambi visiwani Zanzibar ikijiwinda na mechi dhidi ya Botswana kuwania kufuzu fainali za Kombe la Dunia chini ya umri huo zitakazofanyika nchini India baadaye mwaka huu. Mchezo huo dhidi ya Botswana utachezwa Jumapili wiki hii katika Uwanja wa Amaan kisiwani Unguja majira ya saa 10:00 alasiri.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Shime alisema wanaendelea na mazoezi ya kujiandaa na mechi hiyo dhidi ya Botswana kama ratiba ilivyopangwa kwa kujifua asubuhi na jioni.

"Timu inaendelea vizuri na hakuna majeruhi mpaka sasa, wachezaji wote wanafanya mazoezi kwa mujibu wa ratiba, lakini wanapata muda mzuri wa kupumzika," alisema.

Alisema mipango yake mikubwa ni kuona Tanzania inasonga mbele ikiwamo kufuzu kucheza Kombe la Dunia, ndio maana wachezaji wake wanajituma na kufuata ratiba yote iliyowekwa na mwalimu.

Shime alisema katika mchezo huo ambao watakuwa wenyeji, wamejiandaa kushinda nyumbani na baadaye ugenini timu hizo zitakaporudiana.

"Wachezaji wote wanahamasa kubwa ya kufanya mazoezi kwa muda uliopangwa, hali hii inanipa matumaini kuwa timu itafanya vizuri katika michezo yake," alisema Shime ambaye wamekita kambi visiwani Zanzibar akiwa na kikosi cha wachezaji 26.



Kiungo wa Azam FC, Mudathir Yahya (kushoto), akipata upinzani kutoka kwa kiungo wa Coastal Union, Mtenje Juma, wakati akijaribu kuachia shuti timu hizo zilipokutana kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi na kumalizika kwa kutoshana nguvu. **MPIGAPICHA WETU**

## *Azam yataja Coastal ilipowashika Chamazi*

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Coastal Union, Joseph Lazaro, amesema kupata pointi moja dhidi ya Azam FC, ni kufanikiwa kwa mipango yao katika mchezo huo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam.

Hata hivyo, wakati Lazaro akitoa kauli hiyo, Kocha Msaidizi wa Azam FC, John Yona, amekiri kwamba Coastal Union iliwazidi katika nafasi ya kiungo na safu yao ya ulinzi kuwa makini zaidi katika kuzuia.

Wakizungumza baada ya dakika 90 kukamilika kwa timu hizo kutoka suluhu kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu, Lazaro alisema mechi hiyo ilikuwa ngumu kwa sababu walikutana wote wametoka kupoteza na kila mmoja wao akihitaji pointi ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kufikia malengo yake.

"Tumefanikiwa kwa asilimia kubwa, malengo yetu hayakuwa kupata pointi tatu, tumekuja kupata alama moja, ukiangalia tulivyocheza hatukutaka kushambulia zaidi na tulihakikisha tunazuia njia zao za kufunga," alisema Lazaro.

Alisema matokeo ya alama moja ugenini yamerejesha morali ya wachezaji wao wakuwa na matarajio ya kufanya vizuri zaidi katika michezo iliyoko mbele yao.

Kocha Msaidizi wa Azam FC, John aliwapongeza Coastal Union kwa kucheza vizuri na kufanikiwa kuondoka na pointi moja, lakini wachezaji wao kwa kuweza kuwazuia kutapa ushindi.

"Hatukuwa na mchezo mzuri hasa safu ya ushambuliaji tulitengeneza nafasi nyingi, tulishindwa kuzitumia kutokana na kutokuwa makini," alisema John.

Alisema Coastal Union iliwazidi katika safu ya kiungo pamoja na mabeki ambao waliweza kusimama vizuri na kuokoa mipira ya hatari.

## Klabu Bingwa 'Netball' kupigwa Uganda Mei

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mpira wa pete (netball) ya Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati yanatarajiwa kufanyika Kampala, Uganda Mei Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Mpira wa Pete Tanzania (CHANETA), Devota Marwa, alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo yameanza, na tayari wametuma barua kwa klabu husika.

**"Kuelekea mashinda no hayo mpaka sasa tumeshawaandikia barua inayoonyesha tarehe ya mashinda no ili waanze maan dalizi mapema," alisema Marwa.**

Mwenyekiti huyo alizitaja baadhi ya timu ambazo zitashiriki mashindano hayo kuwa ni Uhamiaji, TAMISEMI pamoja na JKT Mbweni.

Aidha, alisema kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, ambayo itafanyika Machi 8, mwaka huu, amejipanga kuutangaza mchezo huo ili kuwajengea uwezo wanawake ikiwa ni pamoja na kuwapa semina ya uongozi kuwawezesha kushiriki michezo mbalimbali.

"Ninaomba wanawake wajitokeze kwa wingi siku hiyo ili tujifunze mambo mbalimbali kutoka kwa wengine," alisema.

## ZISIKUPITE

### CITY WATETA NA HAALAND
KLABU ya Manchester City imefanya mazungumzo na wakala wa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. (***Fabrizio Romano, via Express***)

### CHELSEA SASA KUUZWA
MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich huenda akaiuza klabu hiyo na ofa rasmi inaweza kutoka wiki hii. (***Telegraph***)

### SAKA NA MKATABA MPYA
KLABU ya Arsenal inatarajia kumzawadia mkataba mpya uliiboreshwa mshambuliaji wake wa England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20, mwishoni mwa msimu huu. (***football.london***)

### LEWANDOWSKI HAJAAMUA
MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, hajaamua bado kuhusu hatma yake, lakini amesema yuko tayari kwa uamuzi wowote. (***Sky Sports Germany, via 90min***)

### TCHOUAMENI ATAKIWA BARCA
KLABU ya Barcelona inataka kumsajili kiungo wa Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. (***Sport***)

### RUDIGER MAMBO BADO
WAWAKILISHI wa mlinzi wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, wanaendelea na mazungumza ya moja kwa moja na Real Madrid na PSG. (***Sky Sports***).

### DORTMUND NA HAALAND
BORUSSIA Dortmund haijakata tamaa ya kumbakiza Erling Haaland baada dirisha la usajili la majira ya joto kupita, licha ya Barcelona pia kuonyesha kumtaka. (***Mirror***)

### CHELSEA KUMUUZA BROJA
CHELSEA huenda ikamuuza mshambuliaji wake raia wa Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, na kiungo Faustino Anjorin (20), ili kusaidia kupata fedha za usajili msimu ujao. (***Evening Standard***)

### GUENDOUZI KUBAKI MARSEILLE
KIUNGO wa Arsenal, Matteo Guendouzi atajiunga moja kwa moja kwa mkataba wa kudumu kwenye klabu anayochezea kwa mkopo sasa ya Marseille mwishoni mwa msimu huu kwa ada ya pauni milioni tisa. (***RMC Sport, via Mirror***)

### UNITED YASAKA KOCHA
MKURUGENZI wa soka wa Manchester United, John Murtough amesema mchakato unaendelea kumtafuta kocha wa kudumu wa klabu hiyo. (***Manchester Evening News***)

### WERNER AWANIWA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inawania kumsajili mshambuliaji, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25. (***Sky Germany***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL AGEUKA MBOGO SWALI ABRAMOVICH, URUSI

**●●● Sikiliza, inabidi muache hili, mimi sio mwanasiasa, kiukweli, najisikia vibaya kurudia hii kwa sababu...**

**LONDON,** ENGLAND

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amewataka waandishi wa habari kuacha kumuuliza maswali kuhusu uvamizi wa Urusi nchini Ukraine na mpango wa mmiliki wa timu hiyo kuiacha kwa bodi ya wadhamini.

Tuchel katika kikao na waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa Kombe la FA jana Jumatano kwenye Jiji la Luton, alipoteza ukawaida wake na kuwa na hasira baada kulizwa mara nyingi kuhusu vita ya Ukraine na kitendo cha mmiliki wa klabu hiyo kuaichia timu kwa bodi ya wadhamini baada ya Bunge la Uingereza kutaka awekewe vikwazo.

**"Sikiliza, sikiliza, sikiliza, inabidi muache hili," alisema Tuchel alisema.**

"Mimi sio mwanasiasa inabidi muache hili, kiukweli, naweza kurudia hili tu, naweza kujisikia vibaya kurudia hii kwa sababu, nimependelewa sana, nakaa hapa kwa amani nafanya kadri niwezavyo hapa, lakini naomba muache kuniuliza mimi maswali hayo, sina majibu yake kwenu."

Alipoulizwa ikiwa ana ujumbe kwa mashabiki wa Chelsea kuhusu uamuzi wa Roman Abramovich kuiachia timu kwa bodi ya wadhamini, ambao bado nao hawajakubali, alijibu: "Sina uhakika ikiwa mimi ni mtu sahihi wa kuweza kutoa ujumbe kwa mashabiki kuhusu chochote.

"Tunajaribu kuwa watulivu hapa, na mimi kuwa mtulivu na sisi kuwa watulivu katikati ya majanga au kelele zinazotuzunguka ambazo hatuwezi kuzizuia na hatuwajibiki nazo.

"Ni bora kuwa kimya na kujikita kwenye kile tunachokipenda na kukifanya, huu ndio mchezo."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 985

MECHI KALI
BURNLEY
VERSUS
LEICESTER
1 | 2.91
X | 3.31
2 | 2.42

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# GUARDIOLA: SINA SHIDA GREALISH KUTOFUNGA



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amemtaka Jack Grealish kuacha kujifikiria kuhusu takwimu zake na maoni ya mashabiki kuhusu kutofunga mabao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England, alisajiliwa kwa dau kubwa klabuni hapo la pauni milioni 100 akitokea Aston Villa na amefunga mabao matatu na kutoa asisti tatu katika michezo 25 aliyocheza kwenye mashindano yote.

Grealish alikiri kwamba anataka kuboresha kiwango chake na takwimu zake kwenye klabu hiyo.

"Nadhani kitu kikubwa ni magoli na asisiti hiyo ndiyo lengo na najaribu kufanyia kazi," alisema Grealish akinukuliwa na BBC Sport.

Lakini bosi wa City, Guardiola amesema Grealish anapaswa kuchukua hatua na kuzingatia katika kuisadia timu.

"Labda amekosea. Labda anasikiliza sana kile ambacho watu wanasema. Ni makosa lakini takwimu ni bora na anacheza sawa kabisa, si tatizo lolote," alisema Guardiola akinukuliwa na Sky Sport.

"Amekuja hapa kwa kazi moja tu ya kucheza mpira na kusaidia timu, hayo mengine yeye hatakiwi kusikiliza sana."

# Keane aitaka United imchukue Simeone

**MANCHESTER,** England

ROY Keane anataka kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone kuwa kocha mkuu ajaye wa Manchester United.


Mchezaji huyo wa zamani wa 'Mashetani Wekundu' hao, ambaye ana umri wa miaka 50, aliweka wazi hisia zake kwa kocha ambaye anaona anafaa kuwa na majukumu ya kuinoa timu hiyo wakati akizungumza na na The Overlap Live.

"Labda Simeone, anasifa zinazofaa," alisema Keane.

"Simeone, ni mhusika mkuu. Amefanya mambo makubwa. Ni mhusika mkuu, mtu mkubwa. Hajisumbui na wachezaji. Labda mtu kama yeye akija kwenye klabu anaweza kufanya kazi."

Man United wanapambana kuwa katika kiwango chao kwa muda mrefu baada ya Sir Alex Ferguson kustaafu kwani hadi sasa wameshindwa kumpata mbadala wake sahihi.

Kwa sasa Man United wanajiandaa kukabiliana na mahasimu wao Manchester City Jumapili wiki hii baada ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Watford wikendi iliyopita.



## HABARI MICHEZO

,669,400

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/03/22 | 18:00 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.09 | 3.34 |
| 02. 05/03/22 | 18:00 | Newcastle vs Brighton | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 03. 05/03/22 | 18:00 | Aston Villa vs Southampton | 2.30 | 3.36 | 3.06 |
| 04. 05/03/22 | 18:00 | Norwich City vs Brentford | 2.95 | 3.10 | 2.50 |
| 05. 05/03/22 | 20:00 | Roma vs Atalanta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 06. 06/03/22 | 14:30 | Genoa vs Empoli | 2.61 | 3.26 | 2.71 |
| 07. 06/03/22 | 16:00 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 3.31 | 3.06 | 2.32 |
| 08. 06/03/22 | 17:00 | Reims vs Strasbourg | 3.48 | 2.78 | 2.39 |
| 09. 06/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Troyes | 2.29 | 3.48 | 2.93 |
| 10. 06/03/22 | 17:00 | Bologna vs Torino | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 11. 06/03/22 | 19:00 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 12. 06/03/22 | 19:00 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.38 | 3.21 | 2.91 |
| 13. 06/03/22 | 19:30 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.70 | 3.40 | 2.50 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

ALHAMISI - 03/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 5729 | Maccabi Kishronot Hadera W vs Hapoel Marmorek Rehovot W | 1.61 | 4.30 | 4.90 |
| 14:00 | 3734 | Neroca FC vs Gokulam Kerala FC | 3.42 | 3.37 | 1.96 |
| 14:00 | 5293 | SC Villa vs Busoga United | 1.73 | 3.38 | 4.44 |
| 15:00 | 2599 | FK Mladost Gat Novi Sad vs FK Zeleznicar Pancevo | 2.04 | 3.08 | 3.51 |
| 15:00 | 4625 | FK Imt Novi Beograd vs FK Kabel Novi Sad | 1.27 | 4.45 | 11.61 |
| 15:45 | 1132 | Laci vs Egnatia Rrogozhine | 1.38 | 4.04 | 7.90 |
| 15:45 | 2892 | KS Kastrioti Kruje vs Skenderbeu | 2.21 | 2.89 | 3.32 |
| 16:00 | 1145 | Express FC vs Kampala City Council | 2.90 | 3.00 | 2.60 |
| 16:00 | 1241 | PO Triglias vs SKODA Xanthi | 2.87 | 2.92 | 2.44 |
| 16:00 | 1530 | Al Masry Club vs Enppi Club | 2.39 | 2.95 | 3.15 |
| 16:00 | 2641 | ES Metlaoui vs CS Sfaxien | 6.35 | 2.98 | 1.65 |
| 16:00 | 3498 | Mbarara FC vs Uganda Revenue Authority FC | 3.56 | 3.03 | 2.04 |
| 16:30 | 2125 | Navbahor Namangan vs Nasaf Qarshi | 3.14 | 2.75 | 2.39 |
| 16:30 | 2411 | Bunyodkor vs Sogdiyona Jizzax | 2.13 | 2.75 | 3.76 |
| 16:30 | 3029 | CS Constantine vs CR Belouizdad | 2.09 | 2.98 | 3.51 |
| 17:00 | 1874 | FK Vozdovac vs Red Star Belgrade | 10.57 | 5.19 | 1.23 |
| 17:00 | 3191 | ASK Bravo vs Olimpija Ljubljana | 3.19 | 3.19 | 2.12 |
| 17:00 | 3365 | Shabab Al Dhahiriya vs Markez Tulkarm | 1.53 | 3.85 | 5.38 |
| 17:00 | 4284 | Aizawl FC vs Mohammedan SC | 2.47 | 3.20 | 2.62 |
| 17:00 | 5388 | Chennaiyin FC vs ATK Mohun Bagan | 4.62 | 3.94 | 1.59 |
| 18:00 | 3622 | SP. Braga U23 vs Portimonense U23 | 1.73 | 3.60 | 4.12 |
| 18:00 | 5252 | MS Kiryat Gat W vs Hapoel Beer Sheva W | 1.10 | 8.06 | 14.39 |
| 18:15 | 2388 | Yarmouk vs AL Tadamon | 2.28 | 3.45 | 2.69 |
| 18:15 | 2941 | Lokomotiv Moscow vs Yenisey Kr | 1.24 | 5.00 | 10.58 |
| 18:30 | 5400 | Slavia Sofia vs Beroe | 1.99 | 3.23 | 3.47 |
| 18:45 | 2452 | Vllaznia vs Din. Tirana | 1.55 | 3.42 | 6.16 |
| 19:00 | 3813 | Rubin Kazan vs FC Rotor Volgograd | 1.51 | 3.76 | 5.78 |
| 19:00 | 3836 | Al Ittihad Jeddah vs Dhamk | 1.47 | 4.36 | 6.34 |
| 19:00 | 5783 | Farul Constanta vs Botosani | 1.89 | 3.30 | 4.04 |
| 19:05 | 4966 | Partizan vs Mladost Lucani | 1.09 | 7.71 | 19.27 |
| 19:30 | 4835 | Luka Koper vs Maribor | 3.22 | 3.46 | 2.00 |
| 20:00 | 1574 | Baltika Kaliningrad vs Chayka Peschanokopskoye | 1.51 | 3.61 | 6.17 |
| 20:00 | 1581 | FC Elva vs FCI Levadia Tallinn U21 | 2.01 | 4.06 | 3.07 |
| 20:15 | 2302 | Zenit St Petersburg vs KamAZ | 1.07 | 8.25 | 24.95 |
| 20:15 | 5686 | Maccabi Bnot Emek Hefer W vs Hapoel Raanana W | 1.40 | 4.81 | 5.57 |
| 20:30 | 1182 | Atromitos vs Volos | 1.75 | 3.55 | 4.54 |
| 20:30 | 5970 | Alanyaspor vs Gaziantep BB | 1.86 | 3.37 | 3.76 |
| 21:00 | 1921 | Retro FC Brasil vs Afogados Ingazeira PE | 1.44 | 4.05 | 6.36 |
| 21:00 | 5701 | AS Tel Aviv University W vs Bnot Netanya W | 1.17 | 6.58 | 10.64 |
| 21:00 | 5733 | Al Nasr Riyadh vs Al Hilal Riyadh | 2.52 | 3.42 | 2.62 |
| 22:00 | 1912 | FC Gyori Eto vs Videoton FC | 5.42 | 3.87 | 1.52 |
| 22:00 | 2688 | AZ Alkmaar vs Ajax | 4.44 | 3.86 | 1.62 |
| 22:00 | 4664 | Royal Pari Sion vs FC Universitario de Vinto | 1.30 | 5.19 | 7.31 |
| 22:00 | 5160 | Argesul Pitesti vs Steaua Bucuresti | 4.04 | 3.35 | 1.87 |
| 22:30 | 2723 | Grasshoppers vs FC Lugano | 2.50 | 3.04 | 2.89 |
| 22:30 | 3415 | FC Basel vs St. Gallen | 1.95 | 3.69 | 3.44 |
| 22:45 | 5895 | Anderlecht vs Eupen | 1.27 | 5.48 | 8.61 |
| 23:00 | 1977 | Betis vs Rayo Vallecano | 1.75 | 3.75 | 4.24 |
| 23:15 | 2306 | Tondela vs Mafra | 2.04 | 3.18 | 3.37 |
| 23:15 | 5455 | Everton vs Boreham Wood | 1.11 | 8.30 | 19.76 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# HITIMANA ATAMBA KUTIMIZA LENGO KMC




**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amesema tayari ametimiza malengo yake ya kwanza katika timu hiyo, hivyo kilichobaki sasa ni kuelekeza nguvu na akili yake katika kutafuta pointi tatu kwenye kila mechi ili kuwa miongoni mwa timu zitakazomaliza nafasi tatu za juu mwishoni mwa msimu huu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jana, Hitimana alisema wakati anakabidhiwa timu hiyo, alitakiwa kwanza kuhakikisha anaitoa katika nafasi ya chini, jambo ambalo tayari amefanikiwa na sasa malengo yake ni kuhakikisha wanamaliza nafasi tatu za juu.

Alisema malengo yao ni kupambana kutafuta matokeo na pointi katika kile mechi zilizoko mbele yao ili kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, kila timu inaangalia kushinda mechi zake, ukiangalia msimamo unaona aliyekuwa nafasi ya tatu (Azam FC) anapointi 25, tumepishana na pointi tatu na sisi tuliyokuwa nafasi ya sita kwa pointi 22," alisema na kuongeza:

"Walioko nafasi ya tatu, nne na tano wana alama 24, tunalazimika kushinda mechi zetu ili kutoka hapa tulipo na kupanda katika nafasi za juu," alisema Thierry.

Alisema ana matarajio makubwa ya wachezaji wake wakifuata maelekezo na mbinu za kiufundi na mazoezi anayowapa kwa kuhamishia katika mechi ana imani kubwa ya kufikia yale yanayoyarajiwa.

# Njau kuwanoa wanawake siku yao

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA kilele cha Siku ya Wanawake Duniani itakayoadhimishwa Kitaifa Mlimani City, Dar es Salaam, Machi 8, mwaka huu, Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa (TPBRC), Pendo Njau, ambaye ni refa na jaji wa mchezo huo, amesema anatamani kuwafundisha wanawake wengi mchezo wa ngumi ili wafike alipo yeye.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Njau alisema kupitia kilele hicho ametoa fursa kwa wanawake kujitokeza kufanya mazoezi kila siku kwenye gym ya Japhet Kaseba iliyoko Mwananyamala jijini humo, kuliko kukaa tu nyumbani.

"Kuelekea kwenye kilele cha Siku ya Wanawake, ninawataka wajitokeze kufanya mazoezi ikiwa ni pamoja na kujishughulisha katika shughuli mbalimbali kuliko kuonekana mizigo majumbani," alisema Njau.



Alisema anatarajia kufungua gym yake binafsi kwa ajili ya kuwainua watoto wa kike kupitia mchezo huo na kwamba ataifungua hivi karibuni.

Aidha, aliwataka wanawake wakaze buti kwenye kazi zao ili kupunguza kuharauliwa na wanaume na kuwataka kwa pamoja wajitokeze kuungana pamoja siku hiyo.

# Michezo

Alhamisi Machi 3, 2022

Nipashe




Tuchel ageuka mbogo swali Abramovich UKURASA 21

## ACHENI WAJE...!



Wachezaji wa Simba, mshambuliaji John Bocco (kushoto) na beki wa timu hiyo, Henoc Inonga Baka, wakiwa mazoezini. Simba itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa kesho kuikaribisha Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara mzunguko wa pili. **PICHA: MAKTABA**

## Keane aitaka Utd imchukue Simeone

**MANCHESTER,** England

ROY Keane anataka Kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone kuwa kocha mkuu ajaye wa...



HABARI UK. 22

## Njau sasa kuwanoa wanawake siku yao

**Na Shufaa Lyimo**

KUELEKEA kilele cha Siku ya Wanawake Duniani itakayoadhimishwa...



HABARI UK. 23

# Pablo atangaza vita mpya

## Ni ya kuokota tatu kila mechi, kuanza na Biashara United kesho, asema hakuna namna, lazima...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakianza rasmi kujiwinda kwa mechi za mzunguko wa pili wa ligi hiyo, kabla ya kuialika RS Berkane ya Morocco kwenye mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika hatua ya makundi, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Pablo Franco, amesema kazi ni moja tu kusaka "pointi tatu".

**Simba ilirejea nchini juzi baada ya kutoka kucheza mechi mbili ugenini za Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya USGN ya Niger na kutoka sare ya bao 1-1 kabla ya kwenda Morocco na kuangukia kipigo cha mabao 2-0 dhidi ya RS Berkane.**

Hata hivyo, Simba ambayo ina pointi nne sawa na USGN huku Berkane ikiwa kileleni na alama zake sita na Asec Mimosas ikiburuza mkia kwa pointi tatu, imekuwa timu ya kwanza katika Kundi lao la D, kuambulia pointi ugenini, kwani timu zote zimekuwa zikishinda nyumbani tu na kupoteza ugenini.

Kesho majira ya saa 1:00 usiku miamba hiyo ya Ligi Kuu Bara, itashuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kuikaribisha Biashara United katika mchezo wao wa kwanza katika mzunguko huu wa pili.

Simba ambayo ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 31, 11 nyuma ya vinara Yanga walioko mchezo mmoja mbele, baada ya mechi hiyo ya kesho, Jumatatu itashuka tena uwanjani hapo kuikaribisha Dodoma Jiji FC.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Pablo alisema nguvu na akili zao zote sasa wanazielekeza katika mechi hizo mbili za Ligi Kuu ili kuhakikisha wanaondoka na alama zote sita kabla ya kuikaribisha RS Berkane Machi 13, mwaka huu.

Pablo alisema anatarajia mchezo huo utakuwa mgumu hasa kutokana na ubora wa Biashara United, lakini pia imekuwa kawaida kwa timu ndogo kutoa ushindani mkubwa zinapocheza na timu kubwa.

"Biashara ni timu nzuri na inacheza kitimu, lakini ina wachezaji wazuri na inapocheza na timu kubwa inatoa ushindani mkubwa, lakini kikubwa kwetu ni kuhakikisha tunapata ushindi na uzuri ni kwamba tutakuwa nyumbani," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Alisema malengo yao ni kuhakikisha wanashinda mechi zao ili kupunguza pengo kubwa la pointi kutoka kwa timu inayoongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo, Yanga ili kuweza kutetea taji lao msimu huu.

Kauli hiyo ya Pablo haikutofautiana na ya nahodha wa kikosi hicho, John Bocco, ambaye naye alisema akili zao wamezihamishia katika michezo hiyo miwili kabla ya kuikaribisha RS Berkane mwishoni mwa wiki ijayo.

Bocco alisema tayari wameona tofauti kubwa dhidi ya Yanga walioko kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo na kikubwa kwao ni kuendelea kushinda kila mchezo hadi mwisho wa msimu.

"Tumeona tofauti kubwa ya pointi dhidi ya timu inayoongoza ligi, hivyo kwa sasa tunahitaji kushinda mechi zetu ili kuendelea kuzipunguza na kutoa presha kwao ili kutimiza malengo yetu ya kutetea ubingwa," alisema Bocco ambaye kwa sasa 'gari' limewaka kwake baada ya kuanza msimu kwa ukame wa mabao.

Katika mechi hiyo, Simba imewaeleza mashabiki wake watarajie kuona baadhi ya wachezaji ambao walikuwa majeruhi wa muda mrefu, wakipata nafasi baada ya kuwa fiti kwa sasa.

Wachezaji ambao walikuwa majeruhi ni pamoja na kiungo mkabaji Taddeo Lwanga, ambaye kwa muda sasa amekuwa akifanya mazoezi ya pamoja na kikosi cha kwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >